

**KUCHUNGUZA SIASA NA ITIKADI KATIKA TAMTHILIYA YA NYOTA  
YA TOM MBOYA**

**JOHN ISAACK BATHOLOMAYO KITTO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU  
YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI)  
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## **UTHIBITISHO**

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii itwayo: Kuchunguza wa Siasa na Itikadi Katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya uzamili ya M.A.Kiswahili-Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

-----  
**Profesa, Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

-----  
Tarehe

### **HAKIMILIKI**

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibu wowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

**IKIRARI**

Mimi, **John Isaack Batholomayo Kitto** nathibitisha kuwa, Tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Shahada yoyote.

.....  
Saini

.....  
Tarehe

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu mzazi, mke wangu na watoto wetu wapendwa,  
pia bila ya kuwasahau wataalamu na wanafunzi wote wa fasihi ya Kiswahili.

## SHUKURANI

Kwa hakika si kazi rahisi kuwataja na kuwashukuru kwa majina wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamewezesha kukamilika kwa utafiti huu. Wafuatao wanastahili shukurani za pekee.

Kwanza, napenda kutoa shukurani zangu za dhati Kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehemana Mwenye kurehemu kwa kunijaalia afya njema tangu mwanzo wa masomo yangu mpaka kufikia tamati hii leo.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati na unyenyekevu mkubwa kwa msimamizi wangu profesa, Emmanuel Mbogo kwa msaada wake usio na kikomo uliowezesha kukamilika kwa utafiti huu. Kwa hakika alijitoa sana katika kuniongoza, kunishauri, kunikosoa, kunitia moyo na kunielekeza katika hatua mbalimbali za utafiti huu na hivyo kunilazimu kutumia muda mwingi kutafakarina kufanyia kazi maelekezo yake yaliyosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Nakushukuru sana Profesa Mbogo, kwa dhati ya moyo wangu nakutakia kila lakheri katika maisha yako wewe binafsi pamoja na familia yako MUNGU akubariki sana.

Tatu, Napenda kuwashukuru sana wanataaluma wote wa Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili-Fasihi, hawa ni Dr. Omari Mohamedi, Dr. Elisifa Zelda na Dr. Hilda Pembe kwa kunifundisha, kuniongoza na kunikosoa na hatimayekunijenga kitaalum kwa maana ya pendekezo la utafiti na utafiti wenyewe kwa kuhusianisha mada, malengo, data na nadharia, aidha wataalam hawa wamenijenga katika ujengaji wa

hoja imara na kuitetea ama kuzitetea hoja hizo. Nawashukuru sana wanataaluma wangu.

Nne, natoa shukurani za dhati kwa familia yangu, mke wangu na wanangu wapendwa Flora na Ivona kwa kunivumilia muda wote nilipokuwa masomoni naamini waliniombea muda wote nikiwa mbali na wao lakini namshukuru Mungu nimefikia tamati ya ukamilisho wa utafiti huu. Mungu awabariki sana.

Tano, napenda kutoa shukurani za dhati kwa wanafunzi wenzangu ambao kwa njia moja au nyingine walitoa changamoto mbalimbali zilizosaidia kukamilika kwa utafitihuu. Aidha walinitia moyo na kunihamasisha kwenye masomo yangu Miongonimwaoni Meijo L. Laizer, Gerso Mrua, Georgia Maghiya, Joyce Kaishozi, Mwaftari Japhari, Sarah Mkumbo, Felista Lyimu, Scolastica Mao, Upendo Shayo, Hadija Simba, Farida Saidi, Hawa Nangali, Fernandes Francis na Rugoba Sosthenes. Ahsanteni sana kwa michango yenu.

Mwisho japo si kwa muhimu napenda kumshukuru sana Ndugu Emmanuel Migungakwa kunisaidia namna ya upangaji wa maandishi kwenye komputa na mambo mengine yaliyohusu teknolojia. Mungu akuzidishie uwezo ili uendelee kuwasaidia na wengine.

## IKISIRI

Mada ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza masuala ya siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Lengo kuu la utafiti huu limefikwa baada ya malengo mahususi matatu kukamilika. Malengo hayo ni Kubainisha siasa zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, kubainisha itikadi zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* na kufafanua uhusiano uliyopo kati ya siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Ili kukamilisha malengo haya mahususi, Data za utafiti huu zilikusanywa kwenye kazi teule kwa kutumia mbinu za usomaji na upitiaji nyaraka kwa kina na umakini mkubwa. Aidha data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kinaelezo na nadharia ya U-marx. Utafiti umebaini kuwa, masuala ya kisiasa nayojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ni siasa na harakati za ujenzi wa jamii mpya, uongozi bora na imani kwa wananchi, ukombozi wa nchi za Afrika, elimu na maendeleo, siasa za ukabila, hofu na tamaa ya madaraka, kujitua muhanga, nafasi ya mwanamke katika siasa, uhusiano wa nchi za Afrika na zile za Magharibi, vibaraka wa kisiasa na umwagaji wa damu. Pia utafiti umebaini kuwepo kwa itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kama ifuatavyo: itikadi ya ushirika, ujamaa, mapinduzi, ubepari, kikomunisti, dini, utamaduni, mapenzi na ubaguzi wa kijinsia. Yote haya yatatoa mchango mkubwa katika kuimarisha uongozi wa nchi huru za Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla kwa kuzingatia katiba za nchi zao.



## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO</b> .....	ii
<b>HAKIMILIKI</b> .....	iii
<b>IKIRARI</b> .....	iv
<b>TABARUKU</b> .....	v
<b>SHUKURANI</b> .....	vi
<b>IKISIRI</b> .....	viii
<b>ORODHA YA VIFUPISHO</b> .....	xiv
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
<b>1.0 UTANGULIZI</b> .....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	4
1.4 Malengo ya Utafiti.....	5
1.3.1 Lengo Kuu.....	5
1.3.2 Malengo Mahsusi.....	5
1.5 Maswali ya Utafiti.....	6
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	6
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	6
1.8 Matatizo ya Utafiti.....	7
1.9 Mpangilio wa Tasinifu.....	8
1.10 Hitimisho.....	8
<b>SURA YA PILI</b> .....	9

<b>2.0</b>	<b>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA</b>	
	<b>KINADHARIA .....</b>	<b>9</b>
2.1	Utangulizi .....	9
2.2	Ufafanuzi wa Dhana ya Tamthiliya .....	9
2.2.1	Fani katika Fasihi .....	11
2.2.2	Maudhui katika Tamthiliya .....	13
2.3	Dhana ya Siasa kwa Ujumla.....	15
2.4	Dhana ya Itikadi kwa Ujumla.....	15
2.5	Suala la Siasa na Itikadi katika Tamthilia ya Kiswahili.....	20
2.6	Utafiti Tangulizi kuhusu Siasa na Itikadi katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya.....	22
2.7	Pengo la Utafiti.....	26
2.8	Mkabala wa Kinadharia .....	26
2.8.1	Nadharia ya U- Marx.....	26
2.8.1.1	Sababu ya Kuteua Nadharia Hii .....	33
2.9	Hitimisho.....	33
	<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>35</b>
<b>3.0</b>	<b>MBINU NA ZANA ZA UTAFITI.....</b>	<b>35</b>
3.1	Utangulizi .....	35
3.2	Umbo la Utafiti.....	35
3.3	Eneo la Utafiti .....	36
3.4	Sampuli na Usampulishaji.....	36
3.5	Aina za Data Zitakazokusanywa .....	37
3.5.1	Data za Msingi .....	37

3.5.2	Data za Upili.....	38
3.6	Mbinu za Ukusanyaji wa Data .....	38
3.6.1	Usomaji Makini wa Tamthiliya Teule .....	38
3.6.2	Usomaji wa Nyaraka Mbalimbali .....	38
3.7	Uchambuzi wa Data .....	39
3.7.1	Mkabala wa Kimaelezo .....	39
3.8	Vifaa vya Utafiti.....	40
3.8.1	Kompyuta .....	40
3.8.2	Matini .....	40
3.8.3	Kalamu .....	41
3.8.4	Shajala .....	41
3.9	Usahihi wa Data .....	41
3.10	Maadili ya Utafiti .....	41
3.11	Hitimisho.....	42
	<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>43</b>
<b>4.0</b>	<b>UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA</b>	
	<b>UTAFITI .....</b>	<b>43</b>
4.1	Utangulizi .....	43
4.2	Uwasilishaji na Uchambuzi wa Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya (2016) .....	43
4.2.1	Utangulizi .....	43
4.3	Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data .....	44
4.3.1	Siasa na Itikadi katika Tamthiliya Teule.....	44
4.3.2	Siasa Katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya .....	44

4.4	Hitimisho la Mjadala .....	63
4.5	Itikadi katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya .....	63
4.5.1	Itikadi ya Ushirikina .....	64
4.5.2	Itikadi ya Mapinduzi .....	66
4.5.3	Itikadi ya Ujamaa .....	67
4.5.4	Itikadi ya Ubepari .....	69
4.5.5	Itikadi ya Kikomunisti .....	71
4.5.6	Itikadi ya Dini .....	74
4.5.7	Itikadi ya Utamaduni .....	76
4.5.8	Itikadi Katika Mapenzi .....	78
4.5.9	Itikadi ya Ubaguzi wa Kijinsia .....	79
4.6	Uhusiano Kati ya Siasa na Itikadi Katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya .....	80
4.6.1	Ujenzi wa Uchumi, Mfumo wa Siasa na Itikadi katika Jamii .....	81
4.7	Hitimisho .....	86
	<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>87</b>
<b>5.0</b>	<b>HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>87</b>
5.1	Utangulizi .....	87
5.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti .....	87
5.2.1	Lengo Mahususi la Kwanza .....	87
5.2.2	Lengo Mahususi la Pili .....	90
5.2.3	Lengo Mahususi la Tatu .....	92
5.3	Hitimisho .....	93
5.4	Mapendekezo .....	95

**MAREJELEO ..... 97**

**ORODHA YA VIFUPISHO**

CIA	Central Intelligence Agency
IDS	Institute of Development Studies
KBC	Kenya Broadcasting Corporation
KGB	Komitet Gosudarstvennoy Bezopasnosti (Kwa Kiswahili ni shirika la ukusanyaji wa taarifa za siri ambalo lilikuwa linafanya kazi ndani ya muungano wan chi za kisoviet)
MA	Master of Art
OUP	Oxford University Press
TANU	Tanganyika Afrka National Union
TATAKI	Taarifa ya Taaluma za Kiswahili
TM	Tom Mboya
TPH	Tanzania Publishing House
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TUMI	Taasisi ya Ukuzaji Mitaala
UPE	Universal Primary Education
WET	Wizara ya Elimu ya Taifa
WEU	Wizara ya Elimu na Utamaduni

## **SURA YA KWANZA**

### **1.0 UTANGULIZI**

#### **1.1 Utangulizi**

Sura hii ya utangulizi unajadili kuhusu siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Katika utunzi wake Emmanuel Mbogo, tumeona ametumia sana siasa na itikadi katika tamthilia hii, kwani imetawala kuanzia mwanzo wa kitabu hadi mwisho wa kitabu, lengo kuu ni kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa mantiki hiyo imesababisha mtafiti kuwa na shauku ya kutaka kufahamu ni kwa sababu gani mwandishi huyu ameamua kutumia siasa na itikadi kwa sehemu kubwa katika tamthiliya yake. Aidha sura hii imegawanyika katika sehemu ambazo zinawasilisha kuhusu; usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, matatizo ya utafiti, mpangilio wa tasnifu na hitimisho.

#### **1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Babbie (1999) anasema utafiti ni sayansi ambayo hufanywa kwa kuongozwa na taratibu maalumu ambazo zikifuatwa vizuri hutoa matokeo stahiki pasipo upendeleo wowote. Itikadi ni imani na tafakuri inayoelezea mtazamo wa mwanadamu kuhusu mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu. Kwa mfano, jamii inatakiwa kuwa na mfumo gani wa maisha ili iweze kupata maendeleo na katika mfumo huo kunatakiwa kuwe kwa misingi gani ambayo itafanikisha kupatikana kwa maendeleo. Mathalani katika nchi ya Tanzania, utawala wa kwanza chini ya mwalimu Julius. K. Nyerere

aliamini kuwa ujamaa na kujitegemea ndio mfumo wa maisha ambao utafanya jamii ya watanzania kuwa na usawa na haki kwa watu wote ( Loewestein, 1953).

Kwa ujumla itikadi huongoza jamii na kuifanya jamii hiyo na watu wake wawe wafuasi wa imani ya itikadi fulani ambayo ndiyo inayoongoza jamii hiyo.

Mutembezi (2012) anataja tamthiliya zilizoandikwa na Emmanuel Mbogo mpaka sasa ni *Giza Limeingia* (1980), *Watoto Wetu* (1981), *Tone la Mwisho* (1981), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Morani* (1993), *Sundiata* (1995) na *Fumo Liongo* (2009). Kazi nyingine za hivi karibuni ni *Sadaka ya John Okello* (2015) na *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015) na kwa sasa ni tamthiliya mpya kabisa ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) ambayo ndio imefanyiwa utafiti.

Wamitila (2008) anasema itikadi hutazamwa kama mawazo au mwongozo wa kimawazo unaodhibiti mkabala wa mwandishi kuhusiana na masuala mbalimbali. Dhana ya itikadi inahusishwa kwa kiasi kikubwa na mwanafalsafa wa Ufaransa Destutt de Tracy ambaye aliibuni dhana yenyewe katika miaka ya (1970) kwa maana ya 'sayansi ya mawazo'.

Wapo wanaoangalia itikadi kwa upana zaidi kama jumla ya mawazo ambayo hudhibiti au hujaribu kudhibiti jinsi watu wa jamii fulani inayohusika wanavyoukubali, kuufasiri na kuuelewa ulimwengu wao. Si kila wakati ambapo wanajamii watakuwa na uelewa au ung'amuzi wa itikadi hiyo au kwamba mawazo waliyo nayo ni itikadi.



Kwa maana hiyo, itikadi ni dhana inayorejelea imani, maadili, mtizamo, tabia pamoja na namna ama jinsi ya kufikiri na kuyaelewa mambo mbalimbali sawasawa na kawaida za jamii ambazo huongoza katika namna ya kuamua na kukubali jambo mahsusi. Itikadi ni moja ya kipengele kitakachozungumzwa na mtafiti kwani kimejitokeza sana katika tamthilia ya *Nyota ya Tom Mboya*. Mwandishi Emmanuel Mbogo ameweza kutumia itikadi mbalimbali kama vile mapenzi, mapinduzi, ujamaa, ubepari, dini, utamaduni, ushirikina, ukoinisti, malezi na uzazi. Katika tamthilia hii, mwandishi anaonesha kujikita zaidi katika nadharia ya U-Marx.

Wamitila (2006) anaelezea historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri sio uzalishaji mali hiyo tu bali usambazaji wake. Historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanaakisiwa katika itikadi iliyopo katika jamii, jinsi na miundo ambayo huwa na nguvu kiasi cha wanajamii wasitambue kwa haraka. Ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali. Njia ya kusaidia, hata kuharakisha, kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi ya kibwanyenye inayoimarisha ubepari na nadharia ya Ki-marx inapaswa kuhusishwa na kuandamana na hata kuelezeka kwa matendo ya kiutekelezaji dhidi ya mfumo mzima wa kibepari.

Kipengele hiki bado hakijamakiniwa sana na watafiti wa tamthilia ya Kiswahili hususani tamthilia ya *Nyota ya Tom Mboya*. Katika kuyatalii maandiko na tafiti

mbalimbali mtafiti amebaini kuwa suala la siasa na itikadi limefanyiwa utafiti katika tamthilia mbalimbali isipokuwa *Nyota ya Tom Mboya* ambayo ni tamthiliya mpya kabisa.

TUKI (2014) inabainisha maana ya siasa, kwamba ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi wake, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo au mfumo wa mawazo uongozayo utawala wa serikali ya nchi, kwa mfano siasa ya ujamaa na kujitegemea, siasa ya ubepari na siasa ya ubaguzi wa rangi. Pia inaweza kuwa utaratibu wa utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa. Kwa hakika wataalamu wengi wameshughulikia tamthiliya za Kiswahili katika fani na maudhui kwa jumla kwa kiasi Fulani ambacho hatuwezi kusema ni kikubwa au kidogo bali ni cha katikati. Eneo la siasa na itikadi bado ni bichi kabisa na linahitaji kuchunguzwa ili kuona mchango wa tamthiliya za Kiswahili katika suala zima la siasa na itikadi. Imezoeleka kuona tamthiliya nyingi zikiandikwa na dhamira zikiwa zaidi ni za upendwa na hivyo hata watafiti nao huvutiwa na tamthiliya pendwa na kusahau tamthiliya ambazo zinaeleza masuala dhata kama siasa na itikadi ndio maana sisi tukaamua kutafiti tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* katika eneo hili la siasa na itikadi.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Tom Mboya ni miongoni mwa wanasiasa waliowahi kuwa na jina kubwa katika siasa za nchi ya Kenya na Afrika kwa ujumla. Emmanuel Mbogo (2016) ameandika tamthiliya na kuipa jina la *Nyota ya Tom Mboya*. Utafiti huu unafanywa ili kubaini

namna kipengele cha siasa na itikadi kinavyosawiriwa katika tamthiliya hiyo. Utafiti katika eneo hili haujafanywa vya kutosha kwani ni watafiti wachache tu ikiwa ni pamoja na Ambrose (2014) na Msacky (2015) walioshughulikia siasa na itikadi katika riwaya, Omari (2011) katika ushairi, Shemweta (2015) na Makame (2017) katika tamthiliya. Hii inathibitisha kuwepo kwa pengo la maarifa ambalo ndilo tunaloshughulikia katika tasnifu hii.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Katika utafiti huu mtafiti anaongozwa na malengo mawili, lengo kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

##### **1.3.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu la utafiti ni *kuchunguza masuala ya siasa na itikadi katika tamthilia ya Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo (2016).

##### **1.3.2 Malengo Mahsusi**

Katika utafiti huu kuna jumla ya malengo mahususi kama yalivyoanishwa hapa chini.

- i) Kuelezea masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.
- ii) Kubainisha itikadi zinazojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.
- iii) Kuonesha uhusiano uliyopo kati ya masuala ya kisiasa na kiitikadi yaliyojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*

### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu unaongozwa na maswali yafuatayo;

- i) Ni masuala gani ya *siasa* yanayojitokeza katika tamthilia ya Nyota ya Tom Mboya.
- ii) Ni *itikadi* gani zinazojitokeza katika tamthilia ya Nyota ya Tom Mboya.
- iii) Kuna uhusiano gani kati ya masuala ya *siasa* na *itikadi* katika tamthilia ya Nyota Tom Mboya?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu una umuhimu na mchango mkubwa katika jamii hususani masuala ya siasa na itikadi. Kwa kufanya uchunguzi katika masuala ya siasa na itikadi katika tamthilia teule, baada ya utafiti, utatoa mchango wa maarifa katika nadharia inayofaa kuchambua masuala ya siasa na itikadi. Vile vile, kwa kuzingatia kazi za fasihi, utafiti huu utatoa mchango wa maarifa kwa wasomaji kufahamu jinsi gani siasa na itikadi zinavyoweza kuendesha nchi kiuchumi, kiutamaduni na kijamii, masuala haya yakitumika vizuri, taifa litapata maendeleo lakini siasa na itikadi zikitumika vibaya taifa litaingia katika migogoro na machafuko makubwa. Kuwatambua wanaharakati wa bara la Afrika walivyopigania haki za wanyonge wakiwa na kiu ya kuwaletea maendeleo watu wote bila ubaguzi wa rangi, ukabila wala udini. Aidha utafiti huu utaweza kutumiwa kama rejeleo na hamasa ya tafiti zingine katika tasinia ya fasihi.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza masuala ya siasa na itikadi katika tamthilia ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Mbali na kuandika

tamthiliya, mtunzi huyu pia ameandika riwaya na hadithi fupi. Hata hivyo kwa lengo la kutimiza malengo mahsusi ya utafiti huu, mtafiti amechagua kazi moja tu kati ya tamthiliya alizoandika. Kazi hii ni *Nyota ya Tom Mboya* (2016) ambapo anachambua masuala ya siasa na itikadi. Aidha mbinu ya maktabani imetumiwa katika ukusanyaji wa data. Sababu ya kuchagua kazi hii ni kwa sababu inaonyesha kukidhi malengo ya utafiti huu. Kwa maana hiyo, tamthiliya zingine tofauti na hii hazitahusika katika utafiti huu.

### **1.8 Matatizo ya Utafiti**

Kama kazi yoyote ya kitaaluma haiwezi kukosa changamoto. Changamoto zinapojitokeza hugeuzwa kuwa fursa ya kutatua matatizo. Pamoja na vikwazo vidogo vidogo ambavyo kwa ujumla wake havikuweza kuathiri ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Kwanza kabisa, ni umbali uliopo baina ya mtafiti na msimamizi lakini tatizo hili halikuweza kuathiri ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu kwa sababu tuliweza kuwasiliana kwa njia ya simu na tovuti ambazo ndio njia muhafaka kwetu ya kupashana taarifa.

Aidha, tatizo lingine ni kukosekana kwa marejeleo ya kazi tangulizi na muda mdogo wa kusoma kwa sababu mtafiti anasoma akiwa kazini. Hata hivyo, mtafiti alitumia siku za mwisho wa juma yaani Jumamosi na Jumapili na siku za sikukuu kufanya utafiti. Pia aliwasiliana na wataalamu mbalimbali walioko nje ya wilaya ya Iramba na Mkoa wa Singida kama wanavyo vitabu, majarida na tasnifu ili viweze kumsaidia katika ukusanyaji wa data.

## **1.9 Mpangilio wa Tasinifu**

Mtafiti ameigawanya kazi yake katika sura tano. Sura ya kwanza itatoa utangulizi na kuibua tatizo la utafiti huu, sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu pamoja na mkabala wa nadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zilizotumika kukusanya data za utafiti huu. Sura ya nne inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo ya utafiti na sura ya tano inatoa kwa muhtasari na mchango wa kitaalum na mapendekezo kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

## **1.10 Hitimisho**

Katika sura hii, mtafiti amefafanua vipengele vyote vilivyoonesha haja ya kufanya utafiti huu, aidha utangulizi wa ujumla umejadiliwa kama usuli wa tatizo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, matatizo ya utafiti na mpangilio wa tasinifu. Sura inayofuata imeeleza mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia kinachoongoza utafiti huu.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Mapitio ya kazi tangulizi yana umuhimu sana kwa mtafiti na utafiti. Kombo na Tromp (2011) wanaeleza kuwa kufanya mapitio ya kazi tangulizi humpa mtafiti msingi wa kinadharia, kanuni za utafiti wake kwa kuangalia nadharia walizotumia watafiti waliotangulia. Vilevile kazi tangulizi humpa mtafiti fursa ya kujenga mlingano wa utafiti ambao anataka kuufanya na utafiti ulio tangulia. Mapitio yatajenga uelewa wa mtafiti kujua au kufahamu taaluma iliyofikiwa kwenye eneo la utafiti wake.

Katika sehemu hii mtafiti amejadili kuhusu kazi tangulizi zinazohusiana na mada yake ya utafiti ili kuona watafiti waliotangulia wametafiti nini kuhusiana na lengo ambalo mtafiti amekusudia katika utafiti huu. Katika sura hii imehusu dhana ya tamthiliya, fani na maudhui katika kazi ya fasihi, siasa na itikadi, aidha mtafiti ameitumia nadharia ya U-marx katika utafiti huu.

#### **2.2 Ufafanuzi wa Dhana ya Tamthiliya**

Katika sehemu hii mtafiti amepitia machapisho mbalimbali ambayo yanahusu tamthiliya ili kuona wataalamu watangulizi wameelezea nini kuhusu tamthiliya na kwa mawanda gani. Ili kutimiza lengo lake, mtafiti amepitia machapisho kuhusu fani na maudhui katika tamthiliya ya kiswahili.

Njogu na Chimerah (2011) anasema tamthiliya za Kiswahili zina matumizi kemkem ya nyimbo, ngoma, vitendawili, na hadithi, kama mbinu za kuimarisha na kuindeleza. Katika tamthiliya za Jogoo kijijini na Ngao ya Jadi, kwa mfano, Ebrahim Hussein ameteua hadithi za kimapokezi ili kusimulia kuhusu kubadilika kwa mfumo wa kisiasa na kiuchumi nchini Tanzania.

Muhando (Mlama) na Balisidya (1976:4) kwa pamoja wanakubaliana kwamba, tamthiliya huwa na sifa za kawaida za sanaa za maonyesho. Sifa hizo, kwa mujibu wa watalamu hawa ni: Dhana inayotendeka, Mtendaji, Uwanja wa kutendea na watazamaji lakini Mulokozi na wenzake (1996) wanapingana kidogo kwa kusema, sifa hizo pekee hazitoshi kuipambanua sanaa ya maonyesho na tendo jingine la kijamii ambalo si sanaa, kwa mfano ibada ya kanisani au msikitini, au rabsha ya walevi kilabuni. Hivyo ipo haja ya kusesitiza pia lengo au kusudio la amali inayohusika, muktadha wake, na usanii au ubunifu wake.

Mulokozi (1996) anabainisha kwamba tamthiliya au drama ni fani ya fasihi iliyokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Hivyo, kwa lugha ya kawaida, tamthiliya huitwa mchezo wa kuigiza. Kwa kawaida tamthiliya huwa na masimulizi ambayo huigizwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazogongana. Mgongano huo hatimaye huishia katika mgogoro ambao unaposuluhishwa au kutatuliwa, mchezo huwa umemalizika. Kwa mujibu wa Mlama (1983:203) tamthiliya ni sanaa ambayo huwasilisha, ana kwa ana, tukio fulani kwa hadhira kwa kutumia usanii wa kiutendaji. Kwa mfano badala ya kuwasilisha wazo kwa hadhira kwa kutumia maneno kama katika ushairi, sanaa za maonyesho huliweka wazo lile



katika hali ya tukio linaloweza kutendeka kwa kutumia usanii wa utendaji kama vile vitendo na uchezaji ngoma. Wamitila (2006) anasema tamthiliya ni utungo unaoandikwa kwa mtindo wa mazungumzo. Anaendelea kusisitiza kwamba hii ni hadithi fupi inayowasilishwa jukwaani au kimatendo. Hivyo kujua tamthiliya sio majibizano tu; lazima iwepo hadithi inayosimuliwa.

Bertoncini (1989) anasema tamthiliya ya Kiswahili ni utanzu wa fasihi-andishi katika lugha ya Kiswahili imeanza kushughulikiwa juzijuzi. Mchezo wa kuigiza ulioandikwa ulikuja na wakoloni. Mgeni aliyejikusisha na uigizaji hapo mwanzomwanzo alikuwa Graham Hyslop. Graham Hyslop alifika pande za Afrika Mashariki mnamo mwaka wa 1936 na kuanza kazi ya uigizaji tokea mwaka wa 1944. Katika mwaka wa 1945, alitunga filamu iliyoitwa Akili Mali. Hyslop aliendelea kusimamia mambo ya kimuziki na kimaigizo kwa muda mrefu. Baadaye, aliandika michezo miwili mifupi ya kuigiza mnamo mwaka 1957. Michezo hiyo ilikuwa Afadhali Mchawi na Mgeni Karibu. Kutokana na mawazo ya wataalamu hapo juu tunaweza kusema, tamthiliya ni fani ya sanaa ya maonyesho inayotungwa au kuandikwa ili iigizwe hadharani kwa lengo la kutoa ujumbe fulani, na kutoa burudani. Mambo yanayoitofautisha tamthiliya na fani nyingine za sanaa za maonyesho ni matendo na mazungumzo ya wahusika.

### **2.2.1 Fani katika Fasihi**

Fani ni ule ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi katika kuunda kazi yake ya fasihi kwa namna ambayo itawavutia wasomaji wake wasome au wasikilize kazi yake (Wamitila, 2008). Fani katika kazi ya fasihi hujengwa kwa vipengele vya

wahusika, mandhari, muundo, mtindo na matumizi ya lugha (Njogu na Chimerah, 1999). Watafiti wa tamthiliya huvutika kutafiti aidha mojawapo kati ya vipengele hivi au vyote kwa pamoja kulingana na malengo yao ya utafiti.

Senkoro (1982) anasema “Fani katika fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake,” hivyo na ustadi au ubingwa au mbinu ambazo msanii wa kazi ya fasihi hutumia kuwasilisha kazi ya fasihi.

Mulokozi na Kahigi (1979) hawa kwa pamoja wanasema, “Fani ni sanaa, ni jumla ya vipengele vya lugha vilivyowekwa katika mpangilio mahsusi ili kuto kwetu maana Fulani”. Kwa maelezo haya yanamaanisha kuwa fani ni jumla ya vipengele vya lugha ambavyo msanii hutumia katika kutoa maana fulani kwa hadhira.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988) nao wanaeleza kuwa, “Fani ni umbo lililosanifiwa ili kuelezea hisia za fanani”. Wanaelezea zaidi kwamba fani ni jinsi msanii anavyo finyanga umbo fulani.

Semzaba (2006) anabainisha fani ni mojawapo ya vitu viwili vinavyounda kazi ya sanaa. Umbo livikalo maudhui ndio fani. Anaelezea Wagiriki katika enzi za kabla ya matabaka katika kumwabudu Mungu wa mvinyo na rutuba Dionysus walibuni *dithyramb*. Huu ulikuwa wimbo ambao watu waliimba na kucheza. Wote waliimba na kucheza na hakukuwa na mgawanyo wa waimbaji na wachezaji na wengine kuwa watazamaji. Wote walishiriki wakiwa na wadhifa uliofanana. Jamii ya Wagiriki ikakuwa na kubadikika kuwa ya mabwana na watumwa, umbo la sanaa yao pia

ilibadilika. Fani ya tamthiliya iliyoibuka ilionyesha dhahiri jinsi ilivyofutisha muundo na hali ya maisha ya wakati huo. Maneno badala ya nyimbo yakatumika. Fani ilipoingia Afrika, hasa Tanzania, ilikutana na fani tofauti kabisa zilizosimamia tamaduni tofauti kabisa. Tamthiliya haikuwepo lakini kulikuwa na aina tofauti za sanaa za maonyesho kama vile utambaji, ngoma, miviga na sherehe. Sanaa hizi za maonyesho zilikuwa na mambo yafuatayo: Zilitungwa hapo hapo, hazikuandikwa, hadhira na watendaji walibadilishana na nafasi, hazikuwa kwa biashara, sanaa iliyokama haikuwa ya mtu mmoja bali ya jamii nzima, zilichanganya mambo ya kawaida, ya dini na ujumi pamoja na zilifanwa kwenye duara. Anasema tamthiliya ilipoingia nchini umbo lake lilitofautiana na sanaa za maonyesho za asili. Ilikuwa na mambo yafuatayo: Maandishi, Waigizaji, Hadhira, (Ukumbi, jukwaa, matapo, scenery) mgawanyo dhahiri wa majukumu (kazi) na matumizi ya maneno yanayotakiwa kama kipengele kikubwa.

### **2.2.2 Maudhui katika Tamthiliya**

Maudhui ni jumla ya yale yote ambayo mtunzi wa kazi za fasihi anataka hadhira yake iwapate, iyaelewe na kuwasaidia katika kuendeleza jamii yao (Wamitila, 2002). Maudhui katika kazi ya fasihi hutokana na vipengele vya dhamira, ujumbe, falsafa, migogoro na msimamo wa mwandishi.

Mulokozi (1996) anasema maudhui ni mawazo au mambo yanayosemwa ndani ya kazi ya sanaa. Mtafiti atapitia machapisho mbalimbali yaliyoandikwa na waandishi mbalimbali kuhusu maudhui katika kazi za tamthiliya, lengo kubwa ni kukuza maarifa na kusaidia kukamilisha utafiti / atakaoufanya mtafiti.

Njogu na Chimerah (1999) ni miongoni mwa watafiti na wachunguzi waliochambua dhamira katika tamthiliya za Kiswahili. Wakiichambua tamthiliya ya Mashetani ya Ebrahim Hussein wanasema kuwa tamthiliya hii inahusu mivutano ya kiuchumi baina ya Watanzania na Waarabu. Wanaendelea kueleza kuwa Watanzania wanapambana katika kuondoa ukandamizaji wa Waarabu na kuwa katika misingi imara itakayowasaidia kuinuka kiuchumi na kiutawala. Hata hivyo katika harakati zao za kupambana dhidi ya unyonyaji zinaonekana kutozaa matunda kutokana na baadhi ya viongozi kutokuwa makini katika kuwasaidia wananchi.

Semzaba (2006) yeye anaelezea tamthiliya yoyote ile iwayo lazima iwe na maudhui. Anaendelea kwa kusema, tunaposema maudhui katika tamthiliya tuna maana ya dhamira, msimamo, falsafa, ujumbe, maadili, na vingine vilivyomo. Mara nyingi maana ya tamthiliya haitamkwi waziwazi ila hujulikana kutokana na mahusiano ya wahusika, mawazo wayatowayo, migongano masuluhisho yao. Tamthiliya ilipoingia Afrika hususani Tanzania, maudhui yake yalihusu mambo ya karne iliyopita huko Uingereza. Ni maudhui ambayo yalimstarehesha na kumburudisha mkandamizaji kuyaangalia lakini yalimpumbaza mkandamizwaji. Maudhui ya tamthiliya yalianza kubadilika baada ya mwaka wa 1967. Hali ya uchumi na utamaduni iliyoachwa na mkoloni aliyeondoka ikaanza kupigwa vita. Falsafa iliyojulikana kama Azimio la Arusha ya kukomesha unyonyaji na kuleta uhuru kamili sio kwa Watanzania tu bali Waafrika wote iliwafanya waandishi wa tamthiliya kuandika kuhusu masuala hayo. Tamthiliya kama *Mkwawa Mahinya*, *Tambueni Haki Zetu*, *Kinjekitile* zina maudhui ambayo ni mazao ya itikadi

iliyokuwa ikitawala wakati huo. Tamthiliya hizi zina dhamira ya ukombozi. Dhamira iliyohusu ujenzi wa jamii mpya ambayo ni zao la Azimio la Arusha ilionekana kwenye tamthiliya za *Dunia Iliyofarakana, Mwanzo wa Tufani na Bwana Mkubwa* na zinginezo.

### **2.3 Dhana ya Siasa kwa Ujumla**

Kupitia machapisho mbalimbali mtafiti alisoma dhana ya siasa kama ilivyojitokeza katika machapisho mbalimbali.

Omari (2011) katika tasnifu yake anasema siasa ni sanaa au sayansi ya kutawala na kuongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serikali katika kuongoza na kutawala, serikali hudhibiti maswali yake ya ndani na yale ya nje ili kuleta uwiano sahihi utakaofanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya wananchi. Tunaposema kutawala na kuongoza tuna maana kwamba, siasa ndio huamua hatima ya nyanja nyingine za maisha. Siasa ya nchi ndio inaamua ni aina gani ya uchumi iwepo nchini, mfumo na mpango mzima wa masuala ya kijamii uweje na kadhalika hii ni sawa na mfumo mzima wa maisha ya jamii. Hivyo tunaweza kusema siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi wake, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha jamii hiyo kwa kuzingatia mfumo wa mawazo yaongozayo utawala wa serikali ya nchi. Mtafiti ataichunguza siasa kupitia tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ili iweze kufikia lengo lake alilokusudia.

### **2.4 Dhana ya Itikadi kwa Ujumla**

Itikadi ni dhana ambayo imeelezwa na wataalamu mbalimbali kutokana na ukweli kuwa kila jamii inaongozwa na itikadi fulani katika kufanikisha maisha yake ya kila

siku. Adorno na wenzake (1950) wanaeleza kuwa *itikadi* ni maoni na mwenendo wa kufikiri juu ya maisha ya mwandamu na jamii yake katika vipengele vya siasa, uchumi, dini, utamaduni na masuala ya kijamii kwa ujumla. Hii ina maana kuwa, itikadi waliyonayo wanajamii kuhusu maisha ndiyo itakavyowaongoza katika kufikiri na kutafakari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao kwa maana ya kufanikiwa au kutokufanikiwa. Mawazo haya yanaungwa mkono na loewestein (1953) pale anaposema kuwa, itikadi ni imani na tafakuri inayoeleza mtazamo wa mwanadamu kuhusu mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu.

Wamitila (2006) mtaalamu huyu amelezea dhana ya itikadi ni muhimu katika kazi ya uhakiki, dhana hii changamano imezua mijadala mingi miongoni mwa wahakiki na wasomi mbalimbali. Licha ya kuzungumziwa kwa mapana, dhana hii inabakia telezi kuelezea. Kimsingi, *itikadi* ni uwasilishi wa pamoja wa mawazo, fikra na tajriba hasa ikiwa vitalinganuliwa na uhalisi wa kiyakinifu vinakotengemezwa. Terry Eagleton anapendekeza fasili mbalimbali za dhana hii.

Kwanza, kuelezea njia za kiyakinifu za kijumla za uzalishaji wa mawazo, imani na tathimini katika maisha ya kijamii. Pili, mawazo na imani (za ukweli au uongo) ambazo huashiria mazingira na uzoefu wa maisha ya tabaka maalum la kijamii. Tatu, ukuzaji na uhalalishaji wa matakwa na matamania ya tabaka hilo la kijamii dhidi ya matamania na matakwa kinzani. Nne, kurejelea pale ambapo ukuzaji na uhalalishaji huo unaendelezwa na kundi la kijamii lenye nguvu. Tano, mawazo na imani ambazo husaidia kuhalalisha matamania na matakwa ya tabaka tawala na hasa kwa upotoshaji. Sita, imani danganyifu na potoshi zinazozuka sio kutokana na matakwa ya

tabaka tawala bali kutokana na muundo wa kiuzalishaji wa jamii. Anaendelea kuelezea dhana ya itikadi kwamba ni mawazo au mwongozo wa kimawazo unaoudhibiti mkabala wa mwandishi kuhusiana na masuala mbalimbali. Wapo wanaoangalia itikadi kwa upana zaidi kama jumla ya mawazo ambayo hudhibiti au hujaribu kudhibiti jinsi watu wa jamii fulani inayohusika wanavyokabili, kuufasiri na kuuelewa ulimwengu wao. Si kila wakati ambapo wanajamii watakuwa na welewa au ung'amuzi wa itikadi hiyo au kwamba mawazo waliyo nayo ni itikadi (Wamitila, 2010).

Jilala (2016) anabainisha kuwa itikadi ni mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo fulani wa kiuchumi au kisiasa na kwamba hivyo ndivyo ilivyo, ni mawazo yanayochukuliwa na watu kadhaa na unaweza kusema kwamba mtu fulani binafsi ana itikadi yake. Katika fasihi linganishi, mwanafasihi linganishi anaweza kuamua kuteua itikadi kama kipengele cha ulinganishi ili kuibua kufanana na kutofautiana kwa itikadi ya msanii mmoja na msanii mwingine.

Katika tasnifu yake (Omari, 2011) aliainisha dhana ya itikadi kupitia wataalam mbalimbali, kwa kuanza na Louis Althusser anasema kuwa jamii za kitabaka zinadumishwa na muafaka unaozuliwa na kiitikadi kwa njia mbili kuu. Njia ya kwanza ni kwa matumizi ya vyombo vya kiitikadi vya dola na vyombo kandamizi vya dola. Kwa mujibu wa Althusser, jamii za kitabaka hudumishwa kwa mkubaliano unaopatikana kiitikadi kupitia kwa vyombo vya kiitikadi vya Dola. Vyombo hivi ni kama asasi za kielimu, sheria, siasa, mashirika ya wafanyakazi na jamaa au familia. Vyombo hivi huchangizana na Vyombo Kandamizi vya Dola. Vyombo kandamizi

vya Dola ni asasi ambazo hutumia njia za kugangamiza ili kuwafanya watu (na hasa wafanyakazi) kulitii tabaka tawala. Mifano mikuu hapa ni polisi, magereza na majeshi. Wahakiki ambao wameathiriwa na Michel Foucault hawatilii maanani sana neno 'itikadi' usemi au diskosi.

Marx anaiweka fasihi katika mwanda mpana wa ki-itikadi (wa kikorombwezo) pamoja na dini, falsafa, siasa, sheria, utamaduni, tathmini na sanaa kwa ujumla. Wahakiki wa kifasihi wamezuka na mikabala mbalimbali inayoweza kutumiwa kuonyesha jinsi fasihi inavyohusiana na kuingiliana na uhalisia wa kijamii.

Adorno na wenzake (1950) wanasema itikadi ni maoni na mwenendo wa kufikiri juu ya maisha ya mwanadamu na jamii yake katika vipengele vya siasa, uchumi, dini, utamaduni na masuala ya kijamii kwa ujumla. Hii ina maana kuwa, itikadi waliyonayo wanajamii kuhusu maisha ndiyo itakayowaongoza katika kufikiri na kutafakuri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao kwa maana ya kufanikiwa au kutokufanikiwa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Loewestein (1953) pale anaposema kuwa, itikadi ni imani na tafakuri inayoeleza mtazamo wa mwanadamu kuhusu mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu. Kwa mfano, jamii inatakiwa kuwa na mfumo gani wa maisha ili iweze kupata maendeleo na katika mfumo huo kunatakiwa kuwekwa misingi gani ambayo itafanikisha kupatikana kwa maendeleo. Mathalani katika nchi ya Tanzania, utawala wa kwanza chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamini kuwa ujamaa na kujitegemea ndio mfumo wa maisha ambao utafanya jamii ya Watanzania kuwa na usawa na haki kwa watu wote. Kumbe basi Ujamaa na Kujitegemea ni itikadi na



kama itikadi hiyo ingetekelezwa vizuri jamii ya Watanzania ingeweza kutimiza lengo la kuleta haki na usawa kwa watu wote. Mtaalamu mwingine anayeeleza kuhusu itikadi ni McClosky (1964) anayesema kuwa, itikadi ni mfumo wa imani ambao unaeleza, kujumuisha na kufafanua masuala ya madaraka, haki za binadamu na kutathimini masuala ya kihistoria ili kufanya maamuzi sahihi kwa wakati uliopo na ujao. Hii ina maana kuwa itikadi katika jamii ndiyo inayoeleza namna viongozi wanavyopatikana na ni viongozi wa aina gani wanaohitajika katika jamii husika. Sambamba na hilo pia, itikadi ndiyo inayobainisha haki za binadamu katika jamii hiyo ni zipi na haki hizo zitawafikia vipi watu wanaostahiki kuzipata. Kwa mfano, katika itikadi ya Ujamaa watu wote hutazamwa kuwa ni sawasawa na hakuna mtu mwenye haki zaidi ya mtu mwingine. Inasemwa kuwa, watoto wote wanahaki ya kupata elimu bila ya ubaguzi wa rangi, dini, kabila, jinsia na mahali anapotoka mtoto huyo. Jambo hili linawezekana kuwa hivyo ikiwa jamii inajikita katika itikadi ya Kijamaa kikwelikweli na si vinginevyo (Nyerere, 1973).

Seliger (1976) anasema kuwa, itikadi ni mawazo yaliyobuniwa na watu juu ya namna jamii inavyotakiwa kuzalisha mali na kugawana uzalishaji huo bila kumnyonya mtu yeyote kati ya waliozalisha mali. Mtaalamu huyu anaeleza kuwa katika jamii kuna itikadi mbali zinazohusu uzalishaji mali na namna ya kugawana mali hizo kwa wale waliozazilisha. Ipo itikadi ya ujamaa na kujitegemea inayoamini katika kuzalisha kwa pamoja na kugawana sawasawa kile kilichozalishwa. Pia kuna itikadi ya Kiliberali ambayo inaeleza juu ya mwenye mtaji kuutumia mtaji wake katika uzalishaji na faida inayopatikana ni mali binafsi ya mtu huyo aliyeweka mtaji wake katika uzalishaji. Itikadi hii ni ya

kinyonyaji ambapo kutokana na kusesitiza kwake juu ya faida wafanyakazi walioajiriwa na mtu huyo hufanyishwa kazi nyingi kwa saa nyingi ili aweze kupata faida kubwa zaidi (Smith, 1978). Katika sehemu hii tumejadili kuhusu dhana ya itikadi kama ilivyofafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Kwa jumla, tumeona kuwa wataalamu karibu wote wanakubaliana kuwa itikadi ni imani waliyonayo wanajamii au baadhi ya watu.

## **2.5 Suala la Siasa na Itikadi katika Tamthilia ya Kiswahili**

Sehemu hii imehusu kazi tangulizi zitakazozungumzia suala la siasa na itikadi katika tamthilia ya Kiswahili ili kuona wataalamu watangulizi wametafiti kuhusu nini na nini bado hakijatafitiwa. Lengo hasa la kuwa na sehemu hii katika mapitio ya kazi tangulizi ni kubainisha pengo la kiutafiti lililomsukuma kufanya utafiti huu katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Wapo baadhi ya waandishi walioandikia kipengele cha itikadi kama ifuatavyo: Wafula (2003) ameandika kuhusu suala la itikadi katika tamthiliya ya Kiswahili. Anaeleza kuwa tamthiliya za Kiswahili zinazozungumzia *itikadi* mbalimbali ni zile ambazo zinaeleza visa na matukio yanayohusishwa na mashujaa wa kiutamaduni na kihistoria. Tamthiliya anazozitaja katika kuthibitisha hoja yake ni *Kinjikitile, Mukwawa wa Uhehe, Mzalendo Kimathi na Kilio cha Haki*. Majina ya tamthiliya hizi yanaonesha kuwa ni tamthiliya zinazozungumzia mashujaa kwa sababu hayo ni majina ya watu waliopigana dhidi ya Wakoloni ili kukomboa nchi zao na kuzipatia uhuru. Kwa hali hiyo, tamthiliya hizi zinasawiri itikadi mbalimbali walizokuwa nazo viongozi hao na moja kati ya *itikadi* kuu ilikuwa ni kuleta ukombozi katika jamii zao.

Mulokozi (1996) alijadili kuhusu dhima ya fasihi kwa kuhakiki kazi za wanataaluma mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili kama vile; Aristotle, Immanuel Kant, John Ramadhani, Kezelahabi na Balisidya. Katika mjadala wake alionesha dhima ya Kiitikadi na dhima ya kisiasa.

Katika dhima ya kiitikadi anasema hii inategemea muktadha wa jamii inayohusika, pia nafasi ya mtunzi katika jamii hiyo, na msimamo wake kuhusiana na migogoro na matatizo ya wakati wake. Hivyo fasihi inaweza kuwa na dhima ya kueneza na kuendeleza itikadi inayotawala. Kama tabaka linalotawaliwa ni la wakandamizaji (mamwinyi, mabepari.nk) basi huenda fasihi ya tapo hili ikatetea na kuendeleza maslahi ya tabaka hilo. Mfano maandishi mengi ya kipindi cha ukoloni, kwa mfano *Mashimo ya Mfalme Sulemani, James Mbotela na Uhuru wa Watumwa*. Maandishi hayo yalijaribu kutetea itikadi ya ukoloni kwa kuwaonyesha wakoloni wa kizungu kama watu wema, wachapa kazi, wenye akili nyingi, waliokuja kumkomboa na kumwendeleza Mwafrika. Maandishi yanayosisitiza maadili na utii kwa kawaida huwa yanasaidia watawala kuwadhibiti watawaliwa. Hivyo itikadi ya maandishi hayo ni ya watawala, japo huwa imejificha katika maadili ‘mazuri’. Anaendelea kusema kwamba, Jamii yenye mgawanyiko wa kitabaka au kijumuiya hugawanyika pia kiitikadi. Itikadi ya watawala hugongana na ile ya wanyonge au watawaliwa. Kwa njia hii, mgongano wa kijamii hujitokeza pia katika fasihi.

Kwa upande wa dhima ya kisiasa, mwandishi anabainisha kuwa fasihi imetumika mahali pengi kuendeleza au kuzuia harakati za kisiasa. Wakati wa kudai uhuru

nyimbo nyingi zilitungwa kumsuta mkoloni na kuwahamasisha wananchi wapambane. Kwa mfano, wimbo ufuatao uliimbwa huko Bukoba miaka ya 1950:

*Omungereza ashube owabo  
Twamanyike okuandika  
(Tafsiri yake kwa Kiswahili)  
Mwingereza arudi kwao  
Tumeshajua kuandika*

Nyimbo nyingi za Salehe Mwinamila na Ramadhani “Makongoro” za miaka ya 1950 zilimsuta mkoloni (Songoyi 1988). Nchini Kenya, nyimbo za Mau Mau ziliimbwa kwa kumpinga mkoloni (Maina wa Kinyatti (Mh) 1980).

Baada ya uhuru nyimbo nyingine zilizofanana na kutetea siasa ya chama kinachotawala, kwa mfano siasa ya ujamaa nchini Tanzania. Nyimbo nyingine nyingi huimbwa ili kuchochea uzalendo miongoni mwa wananchi, kwa mfano wimbo mashuhuri wa “Tanzania, Tanzania”:

*Tanzania, Tanzania  
Nakupenda kwa Moyo Wote  
Nchi yangu Tanzania  
Jina lako ni tamu sana;*

Aidha hadithi na tamthiliya huweza kutumika kueneza ujumbe wa kisiasa. Mfano mzuri ni tamthiliya ya Alamin Mazrui ya *Kilio cha Haki* ni mfano wa igizo lililohubiri siasa ya kupinga ubepari.

## **2.6 Utafiti Tangulizi kuhusu Siasa na Itikadi katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya**

Mtafiti atapitia machapisho ya waandishi mbalimbali yanayohusiana na siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.

Mlama (1991:154-155) katika uhakiki wake kuhusu itikadi za jadi, alibaini kujitokeza katika tamthiliya kadha, kama vile, *Njia panda* (Mhanika), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (Mbogo), *Kinjekitile* (Hussein) na *Mafarakano* (Kitsato). Kwa ujumla uganga na itikadi za jadi katika tamthiliya hizi zinasawiriwa kama amali muhimu za jamii zifaazo kutumiwa kutanzulia baadhi ya matatizo ya kimaisha. Katika baadhi ya tamthiliya za “Thieta ya Umma” uchawi na itikadi za “ushirikina” zinaonyeshwa kama tatizo sugu lenye kukwamisha maendeleo.

Wafula (2003) mtaalam huyu alifanya uhakiki kuhusu tamthiliya, historia na maendeleo yake. Katika uhakiki wake alichunguza tamthiliya mbalimbali, miongoni mwa hizo alichunguza tamthiliya ya *Visiki* (Khaemba Ongeti) ambayo inafanana na tamthiliya za *Nitaolewa Nikipenda na Kesho Wakati Kama Huu* (Ngugi) zote zinawatetea mafukara wa ulimwengu. Katika tamthiliya ya *Visiki* imewachora wahusika muhimu Matanga na Huzuni, hawa ni maskwota ambao hapo zamani walishiriki katika vita vya ukombozi wa nchi yao. Baada ya uhuru, Matanga na Huzuni wana imani kwamba miongozo ya maendeleo na maongezi ya kisiasa yatawawezesha kubainisha nafasi zao katika taifa lao huru. Kinyume na matarajio yao, viongozi wanaochipuka baada ya uhuru ni walafi, wachoyo na wenye kujitakia makuu. Pamoja na kuwanunua watu maskini ili watu hao wawapigie kura, wanafuata mifumo ya kisiasa na kiuchumi isiyowafaidi watu wa kawaida. Katika kuchunguza tamthiliya na itikadi Wafula alisema, itikadi ya ujamaa imewaathiri wanasanaa wengi wa Afrika ya Mashariki. Katika tamthiliya za *Mkwawa wa Uhehe* (1979) na *Kilio cha Haki* (1981). Waandishi hawa wanaamini kwamba mikinzano kati ya matabaka tawala na matabaka tawaliwa ndiyo msingi wa maendeleo ya kizazi cha mtu. Hata

hivyo, misisitizo ya Mulokozi na Mazrui hailingani katika hali zote. Mulokozi anatilia mkazo mikinzano ya kihistoria ilhaji Mazrui anamulika nuru miamko ya watu binafsi inayowaongoza kuchukua misimamo maalumu juu ya maisha.

Ntarangwi (2004) yeye alihakiki kazi za fasihi na kugusia suala la itikadi, ambapo anaelezea kwamba humaanisha yale anayoyaamini mtu, ambayo humwezesha kutizama na kuelewa maisha yaliyomzunguka katika ujumla wake; ni mambo anayoyakubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopaswa kuzingatia na kuheshimu. Itikadi ni imani aliyonayo mtu kuhusu mambo ya maisha. Ni jambo la msingi katika fasihi kwani ni kigezo cha kupima na kutathimini kazi ya fasihi fulani kwa upande wa usomaji au mhakiki. Anaendelea kwa kubainisha itikadi ni dira ya kupima ni mambo gani mwandishi anapaswa kuchagua kuandika na ni kwa madhumuni gani. Kwa upande wa mwandishi itikadi ndiyo humwezesha kusawiri wahusika wake vilivyo ili wakubalike katika utunzi fulani. Itikadi ni muhimu sana katika kuitazama kazi ya mwandishi, kwani ni vigumu kutoa uchambuzi na uhakiki wa kazi za fasihi. Berg (2009) anaeleza kwamba ni katika utalii wa kitaaluma ndipo pengo la utafiti hubainishwa na kufanyiwa utafiti na kuliziba. Hivyo basi, katika sehemu hii hupitiwa kazi tangulizi ambazo zinaendana na mada ya utafiti ili kubainisha pengo la kiutafiti lililoachwa na watafiti watangulizi. Baadhi ya wataalamu wa fasihi walifanya utafiti na kuhakiki kazi mbalimbali kuhusu masuala ya siasa na itikadi kama ifuatavyo:

Njogu na Chimera (2011) hawa walitafiti kwa kuonyesha ni jinsi gani unaweza kupanda ngazi na kushuka kama taashira ya migogoro ya kisiasa katika muktadha wa tamthiliya ya *Mashetani*. Katika tamthiliya ya *Mashetani* iliyoandikwa na Ebrahim

Hussein ameonyesha ni kwa namna gani uchumi na Siasa vinaingiliana. Tamthiliya hii imejengwa kutokana na mvutano baina ya makundi mawili ya watu waliokuwa na madaraka na wanaoanza kupata madaraka. Anaendelea kufafanua kwamba baada ya mataifa mengi ya Afrika kupata uhuru, viongozi fulani hutumia nafasi zao za kisiasa kujilimbikizia mali na kuwasahau wananchi wa kawaida. Anasema Visiwani Zanzibar, kulitokea mapinduzi mwaka 1964 dhidi ya utawala wa kisultani. Mashamba makubwa makubwa yalitaifishwa, na baadhi ya viongozi waliokuwa katika tabaka la juu wikalazimika kutoroka nchini.

Omari (2011) katika tasnifu yake iliyochunguza siasa katika ushairi wa *Kezilahabi* kupitia diwani ya karibu *Ndani (1988)* na *Dhifa (2008)* anasema *siasa* ni sanaa au sayansi ya kutawala na kuongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serikali katika kuongoza na kutawala, Serikali hudhibiti maswala yake ya ndani na yale ya nje ili kuleta uwiano sahihi utakaofanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya wananchi. Hivyo basi, tunaposema kutawala na kuongoza tuna maana kwamba, siasa ndio huamua hatima ya Nyanja nyingine za maisha. Siasa ya nchi ndio inaamua ni aina gani ya uchumi iwepo nchini, mfumo na mpango mzimz wa masuala ya kijamii uweje na kadhalika. Hii ni sawa na kusema kwamba, si rahisi kutenganisha siasa na mfumo mzima wa maisha ya jamii.

Ambrose (2014) katika utafiti wake uliochunguza masuala ya siasa katika riwaya za Shaaban Robert yaani *Kusadikika* na *Kufikirika*, Shaaban Robert ameeleza masuala mbalimbali ya kisiasa ambayo yana umuhimu mkubwa katika maendeleo ya mataifa

machanga kama ilivyo Tanzania masuala hayo ni uongozi katika jamii, uongozi mzuri na uongozi mbaya.

## **2.7 Pengo la Utafiti**

Baada ya mtafiti kutalii machapisho, majarida na tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalamu wa fasihia alibaini kuwa utafiti unaohusu masuala ya siasa na itikadi umefanyika kwa kiasi kidogo sana hivyo bado ni tete hususani tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) ambayo ni mpya kabisa haijafanyiwa utafiti. Kwa mantiki hiyo mtafiti aliona kuwepo kwa mwanya, ndipo aliamua kuziba pengo hilo kwa kufanya utafiti kwa kina ili kufikia lengo alilokusudia.

## **2.8 Mkabala wa Kinadharia**

Katika utafiti huu, mtafiti atatumia nadharia ya U-marx. Nadharia hii itatumika kama nyenzo muhimu katika kuchambua suala la siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo.

### **2.8.1 Nadhaira ya U- Marx**

Katika sehemu hii mtafiti, ataperuzi machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nadharia ya U-marx, waasisi, misingi ya nadharia hii, historia yake na umuhimu wake katika utafiti huu.

Bila shaka nadharia hii itakuwa ya msaada mkubwa kwa mtafiti katika kufanikisha uchambuzi wa data ya masuala yanayohusu siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.



U-maksi (Marxism) ni falsafa ambayo inafuata uyaikinifu na inakusudia kuleta maendeleo ya haraka katika jamii kuanzia uchumi unaotazamwa kuwa msingi wa mahusiano yote. Lengo kuu ni kuondoa matabaka katika jamii na kuleta usawa kati ya binadamu. Njia ni kuwawezesha wanyonge kudai haki zao kwa kuungana na kuleta mapinduzi dhidi ya wanyonyaji. Waanzilishi ni Mjerumani Karl Marx na Mwingereza Friedrich Engels uliendelezwa karne ya 20. Baadhi yao walioendeza ni Joseph Stalin wa Urusi na Mao Zedong kutoka China.

Senkoro (1987) mhakiki huyu wa kazi za fasihi anasema unapoichambua kazi ya fasihi ni vema kuihusianisha na nguvu mbalimbali za jamii kwani ndizo zilizoizaa kazi hiyo. Katika kufanya hivyo, uhakiki wa U-marx husisitiza pia kuhusu masuala ya itikadi, hasa kuhusu utabaka wa jamii, na athari zake katika uundaji wa kazi ya sanaa, kwani, kufuatana na uhakiki huu, kila msanii ni mwakilishi wa tabaka fulani kwa kupenda au la, kwa kujua au kutokujua.

Ntarangwi (2004) anasema kwamba, mhakiki wa Ki-marx hukita nadharia yake kwenye itikadi za Karl Marx na Fredrick Engles, na hasa kwenye madai ya hao wawili kuwa, katika tathimini ya mwisho kabisa maendeleo ya historia ya binadamu pamoja na taasisi zake, yatakuwa ni tokeo la mabadiliko katika njia za kimsingi za uzalishaji mali. Kwamba mabadiliko kama hayo husababisha mageuko katika muundo wa matabaka ya kijamii ambayo katika kila kipindi huendeleza kung'ang'aniwa kwa uwezo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii; na kwamba dini, fikra na utamaduni wa jumuiya yoyote (zikiwemo sanaa na fasihi kwa kiwango fulani) huwa ni itikadi na miundo maalum ya kitabaka ambayo ni zao la miundo na

matabaka ya kijamii yaliyomo wakati huo. U-marx huchukua kwamba jamii zote za kitabaka huzalisha mkururo wa miundo ya urazini inayokinzana na kushindana. Katika jamii ya kibepari, kwa mfano, aina tofauti za mitizamo kuhusu maisha huwakilisha haja tofauti za kitabaka ambazo hutegemea hasa mikinzano kati ya mapato na nguvu za kutenda kazi. Kwa hivyo Umarx huhusisha itikadi na uzalishaji mali na jukumu lake katika mivutano ya kisiasa katika jamii. Jinsi watu binafsi wanavyoelewa msingi wa maisha yao hutokea kuwa kamba ya mvutano ambapo wanaweza ama kubadilika au kuendelezwa. Kwa mfano, chini ya mfumo wa kibepari, wafanyakazi wanashurutishwa kuuza uwezo wao wa kufanya kazi kwa wale wanaotawala mazao pamoja na huduma. Wanaotawala nguzo za uzalishaji mali hunufaika kupitia kwa dhamana ya ziada iliyozalishwa na wafanyakazi. Hii ni kati ya mali inayobakia baada ya kuondoa matumizi ya malighafi, mashine, na nguvukazi. Faida hupatikana kwa kuwalipa wafanyakazi malipo ya chini kuliko dhamana ya kazi waliyofanya.

Wamitila (2006) katika uhakiki wake ameelezea nadharia ya U-marx kuwa unahusu Nyanja mbalimbali kama uchumi, historia, jamii na mapinduzi. U-marx una sifa ya kijumla inayojitokeza katika mwelekeo wake wa kuligusia kila eneo, na kuwa na la kusema kuhusu takribani kila kitu ingawa hili huonekana kama udhaifu na wapinzani wake. Kwa ujumla huo wa kimkabala ndio msingi wa baadhi ya wahakiki kuongea juu ya nadharia za ki-Marx.

Mawazo ya Karl Marx kuhusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. U-marx ni falsafa ya kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo

mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. U-marx haitegemezi mfumo wake wa kifalsafa kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali anayeyategemeza kwenye uhalisi unaoonekana. Katika mambo yafuatayo yanachunguza mawazo ya kimsingi katika nadharia hii ambayo hutokeza kwenye mikabala hiyo tofauti.

Kwanza, historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelekeza katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri sio uzalishaji mali hiyo tu bali na usambazaji wake. Suala hili la uzalishaji mali na usambazaji wa mali hiyo linaunda kile ambacho hujulikana kama ‘msingi’. Kwenye msingi huo ndiko kunakotengemezwa muundo wa juu au ‘kikorombwezo’ ndicho kinachohusisha maadili, itikadi, dini na utamaduni.

Sifa za kikorombwezo zinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na msingi. Hata hivyo mabadiliko yanayotokea katika muundo wa kikorombwezo, kama mageuzi katika muundo wa kiutawala, huweza kuuathiri msingi. Wahakiki wanaotilia mkazo sana kwenye msingi na kusema kuwa una athari kuu wanahusishwa na ‘U-marx pujufu.’ Hawa wanaamini kuwa msingi unaathiri vipengele vyote vya maisha ya kijamii. Baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa mabadiliko yanayotokea katika kikorombwezo kama muundo wa *kisiasa* yanaweza kuathiri au hata kuharakisha kubadilika kwa msingi.

Pili, wahakiki wa Ki-marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi – jamii.

Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka, je harakati hizi zinasababishwa na nini? Katika *The German Ideology*, Marx na Engels walisema kuwa kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine.

Tendo la kwanza la kihistoria kwa hiyo ni kutafuta njia ya kuyakidhi mahitaji haya ya kimsingi. Ili kufanikiwa katika lengo hilo, binadamu hulazimika kujiunga pamoja na kuunda umoja ili kuimarisha ubora na wepesi wa kuizalisha mali ya kukidhi mahitaji hayo. Muungano huo huwa na ugawaji wa majukumu au kazi ambayo ndiyo msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii. Hatua ya juu ya maendeleo huu ni uzukaji wa mfumo wa ubepari. Katika mfumo huu, mali inamilikiwa na idadi ndogo ya watu. Watu hao wanaipata mali yao kutokana na unyonyaji wa umma na hasa wafanya kazi.

Kadri mfumo wa ubepari unavyoendelea ndivyo ubora wa uzalishaji mali unavyoongezeka na tofauti kati ya matabaka kuimarika kwa kuwa kuna watu wanaofaidika kwa njia zisizo za haki. Kufaidika huko kwa njia zisizo za haki, pamoja na mbegu za kujiangamiza zilizomo kwenye mfumo wa ubepari, vinachangia kuuangusha mfumo wenyewe. Marx anaamini kuwa haya yanatokana na mfanyiko wa kiasilia wa kihistoria. Mfanyiko huo ni wa kipembuzi. Kwa mujibu wa mawazo haya, historia huendelea kutokana na ‘mfululizosafu’ wa mkinzano wa mawazo. Matokeo ya mkinzano huo ni kuzuka kwa hatua nyingine mpya ya kihistoria. Huu ndio msingi wa kile kinachoitwa ‘upembuzi wa kiyakinifu.’

Tatu, matamaniao na matakwa ya matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanakisiwa katika *itikadi* iliyopo katika jamii, jinsi na miundo ya mawazo ambayo aghabu huwa huenda wanajamii wasiitambue kwa haraka. Tunaweza kusema kwa kuitumia istilahi ya kisaikolojia, kuwa haya yamo katika ‘ung’amuzibwete wa jamii’ inayohusika. Fasihi inayojitokeza inaweza kuyaakisi au kuyadhihirisha mahusiano ya nguvu katika jamii.

Nne, kuhusiana na mawazo yaliyopo hapo juu, wahakiki wanaamini kuwa ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali kutokana na juhudi za wafanyakazi au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizo unazozisheheni.

Tano, njia ya kusaidia na labda hata kuharakisha, kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua batili iliyopo katika itikadi ya kibwanyenye inayoimarisha ubepari. Hili linakuwa jukumu muhimu la waandishi wa kifasihi. Kazi zenye mwelekeo huo zitafichua ubaya na uovu wa mfumo huo kama tunavyoona kwenye riwaya ya *Pepo ya Mabwege* ya H. Mwakymbe na riwaya ya mwandishi maarufu, Ngugi wa thiong’o, *Shetani Msalabani*.

Sita, nadharia ya Ki-marx inapaswa kuhusishwa na kuandamana pamoja na hata kuelezeka kwa matendo ya kiutekelezaji dhidi ya mfumo mzima wa kibepari.

Nadharia yoyote ya kihakiki huwa na dhana za kimsingi ambazo ni muhimu katika uchunguzi wake. Katika utangulizi, tulidokeza kuwa haiwezekani kuyazungumzia

masuala yote kuhusiana na nadharia yoyote ile. Hii ni kwa kuwa nadharia za kihakiki zina upana mkubwa na nyingine hubadilika kila uchao. La msingi hapa basi ni kujifunga kwa dhana zilizo muhimu kabisa.

Dhana ya kwanza ni ukengeushi. Karl Marx anasema kuwa ugawaji wa kazi unaishia kuusababisha utengano fulani kati ya wanaohusika au binadamu. Hii ni hatua kimsingi ya 'ukengeushi.' Mfumo wa kibepari unapoendelea kuboreka unasababisha hali ambapo uhusiano uliopo kati ya mfanya kazi na tokeo la nguvu zake ni wa kitu kigeni (*alien object*) watu wanaishia kukengeushwa na jamii yao kutokana na mfumo wa kianisho (specialization) unaosisitizwa na kukuzwa na ubapari.

Dhana nyingine muhimu katika uhakiki huu ni 'ubidhaaishaji.' Marx anaitumia dhana ya; bidhaa' kukielezea au kukirejelea kitu kinachozalishwa sio kwa nia ya kutumiwa bali kubadilishwa katika mfumo wa kibepari wa soko. Bidhaa hizo hazitathminiwi kutokana na kazi yake bali ni kutokana na bei zinazoweza kuvuta. Yaani msingi wa kuzitathmini thamani kimatumizi bali ni thamani kimabadilishano. Katika msingi huu, bidhaa zinaishia kuhusisha nguvu au kani fulani fiche ambazo huwavuta watu na kuwafanya wawe na mvuto mkubwa wa kukimiliki kitu fulani ambacho kinawasisimua. Huu ndio msingi wa 'kuabudu bidhaa' (*fetishism of commodities*).

Hii ni sifa kuu katika mfumo wa kibepari na ni msingi wa uchumi wa kibidhaa ambapo watu husukumwa na kani za kununua na kumiliki vitu ambavyo labda hawavihitaji au wanavikinai haraka na kutamani vingine. Sifa hii ya ubidhaaishaji

inaishia kuwahuu binadamu ambao hawathaminiwi kama binadamu ila kutokana na uwezo wa kuzalisha mali. Dhana hii ya ubidhaaishaji inaingiliana na nyingine iitwayo ‘udude’ (*reification*) iliyosisitizwa na Lukacs. Dhana hii inarejelea hali ya kuwafanya binadamu sawa na vitu au kuwadhalilisha na kuwafanya vitu visivyokuwa na thamani.

### **2.8.1.1 Sababu ya Kuteua Nadharia Hii**

Mtafiti ameamua kutumia nadharia ya Umarx kwa sababu ni nadharia ambayo inafaa kulingana na malengo ya utafiti. Kama ilivyoielezwa hapo awali kuwa lengo la utafiti huu ni kuchunguza siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ambayo imeandikwa na mwandishi mashuhuri wa fasihi Emmanuel Mbogo. Nadharia hii itajibu malengo mahususi ambayo yameainishwa na mtafiti. Kwa kutumia misingi ya nadharia ya Umarx, mtafiti ameona kuwa nadharia hii itamuongoza katika kuchunguza na kubaini siasa na itikadi badala ya kutumia nadharia zingine za fasihi. Aidha, nadharia hii inaonekana kufaa katika kujadili data za utafiti huu utakaohusu itikadi, siasa na aina zake zinazojitokeza katika tamthiliya teule.

## **2.9 Hitimisho**

Katika sehemu hii mtafiti ameyafanya mapitio ya kazi tangulizi kwa kupitia machapisho na tafiti mbalimbali kuhusu mada yake ya utafiti. Mtafiti ameamua kufanya utafiti huu baada ya kubaini kuwa, ipo haja ya kufanya utafiti huu kwa sababu kuwa hakuna utafiti uliofanyika kwa lengo la kuchunguza suala la siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Aidha, katika sehemu hii amebainisha nadharia ambayo imeitumika kama kiunzi cha uchunguzi, uchambuzi na

kujadili data na matokeo ya utafiti huu. Nadharia hiyo ilichanganua ili kukamilisha katika kufukia malengo ya utafiti wake ambao ni kubaini masuala ya siasa, itikadi na uhusiano uliopo kati ya siasa na itikadi katika tamthiliya *Nyota ya Tom Mboya*.



## **SURA YA TATU**

### **3.0 MBINU NA ZANA ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Katika sura hii mtafiti amewasilisha na kujadili mbinu za utafiti zitakazotumika katika utafiti wake. Kwa kuzingatia umuhimu wa kutumia mbinu za utafiti. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti wa kitaaluma kwa sababu ni kutokana na mbinu hizo ndipo utafiti huo wa kitaaluma ufanyike kisayansi na si vinginevyo. Kwa hiyo, katika sura hii mtafiti atajadili kuhusu umbo la utafiti, eneo la utafiti, aina za data, mbinu za ukusanyaji, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

#### **3.2 Umbo la Utafiti**

Umbo la utafiti ambalo wakati mwingine hufahamika kama usanifu wa utafiti hutoa picha kamili inaoonesha namna na jinsi utafiti ulivyofanyika tangu mwanzo mpaka mwisho wa utafiti (Kothari, 2008). Umbo la utafiti ndilo linaonesha kuwa utafiti husika ulikuwa ni wa namna gani na data zilikusanywa vipi. Robson (2007) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni umbo la utafiti ambalo lina faida nyingi kwa mtafiti. Kwanza umbo hili la utafiti humwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa kushughulikia jambo ambalo tayari analijua tofauti na kufanya utafiti bila kujua nini hasa unashughulikia. Mtafiti hatapoteza muda kwa kusoma tamthiliya nyingine bali atamakinikia alizoziteua na nyingine atazisoma kama sehemu ya kujaziliza data zake. Pili, umbo hili la utafiti humsaidia mtafiti kuchunguza jambo kwa kina na kulitolea mahitimisho yanayostahili. Zipo aina

nyingi za umbo la utafiti lakini mtafiti wa kazi hii ameamua kuchunguza siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Mtafiti ameteua tamthiliya hii ambayo ndiyo ataishughulikia kwa kina na kuwezesha kukamilisha lengo lake la utafiti.

### **3.3 Eneo la Utafiti**

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti utafanyika kulingana na vile mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti (Creswell, 2009). Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika ili kukusanya data za utafiti kwa lengo la kukamilisha malengo mahususi ya utafiti (Kothari, 2008). Hivyo eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la mtafiti na kwamba eneo au maeneo ambayo yanateuliwa ni lazima yaweze kutoa data za kukamilisha malengo mahususi ya utafiti. Mtafiti alifanyia utafiti wake katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ambapo ndiko alipolizipatia data za msingi.

### **3.4 Sampuli na Usampulishaji**

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa na kuwa ndio wakilishi wa kundi hilo lote (Keys, 1980). Sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti hueteua akiwa na imani kwamba, itampatia data itakayowezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake (Newman na Wenzake, 2006:22). Kwa msingi huu basi, sampuli lengwa/kusudi katika utafiti huu ni tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo. Mtafiti ameteua kazi hii kwa kuwa anaamini kwamba, itampatia majibu ya maswali yake katika utafiti na kukamilisha malengo mahususi. Pamoja na hayo, sampuli haiwezi kupatikana bila ya kufanyika

kitendo cha usampulishaji. Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha watu ili kitumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa pale ambapo sio rahisi kutafiti zima (Bryman, 2004). Hivyo usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo itawaklisha watafitiwa wote wanaolengwa katika utafiti unaotarajiwa kufanyika. Mtafiti ametumia mbinu ya usampulishaji lengwa katika kupata data za utafiti wake. Emmanuel Mbogo ameandika tamthiliya nyingi, lakini mtafiti amelenga tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kwa kuamini kwamba, kitabu hiki kitampatia data alizozihitaji na kuweza kukamilisha malengo mahususi ya utafiti wake. Data zilizokusanywa zilihusu masuala ya siasa na itikadi.

### **3.5 Aina za Data Zitakazokusanywa**

Kimsingi katika utafiti huu, mtafiti amekusanya data za aina mbili, amekusanya data za msingi na data za upili.

#### **3.5.1 Data za Msingi**

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza, na hujulikana kama data halisi ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huo anaokusudia kuufanya ( Good, 1966). Data za msingi huwa ni ghafi na hukusanywa kwa lengo la kuziba pengo la utafiti lililoachwa na watafiti wengine waliotangulia (Kombo na Tromph, 2006).

Kothari (1992:95) anasema kwamba, data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi. Mtafiti atazikusanya data za msingi katika utafiti wake kutoka katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.

### **3.5.2 Data za Upili**

Mtafiti atazipata data za upili ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti wengine ambazo zitamsaidia kujibu maswali ya utafiti wake. Data za aina hii atazipata katika Makala, vitabu, majarida, tovuti, tasnifu na machapisho mbalimbali ambayo.

## **3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data**

Mtafiti ametumia mbinu ya maktabani katika kukusanyia data za msingi ili ziweze kukamilisha kile anacho kifanyia itafiti.

### **3.6.1 Usomaji Makini wa Tamthiliya Teule**

Usomaji wa kina ni mbinu ya kukusanya data za msingi katika matini kama vile riwaya, ushairi na tamthiliya kwa lengo la kupata data zitakazokamilisha malengo ya utafiti unaokusudiwa kufanywa (Kothari, 2008). Utafiti huu ulihusisha kukusanya data kutoka katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* ambayo ilimtaka mtafiti kuisoma tamthiliya hiyo kwa kina ili kufanikisha upatikanaji wa data.

### **3.6.2 Usomaji wa Nyaraka Mbalimbali**

Young (1984) anasema mbinu ya upili ni mbinu ya kukusanya data mezani. Yaani mtafiti huenda uwandani kuhoji au kufanya mahojiano na watafitiwa. Itambidi mtafiti kusoma machapisho mbalimbali katika maktaba ili imsaidie kupata data za upili. Maktaba ni sehemu muhimu sana katika kupata vyanzo mbalimbali vya data za kimaelezo kwa sababu mtafiti atafanya uchunguzi wa kina muktadha wa tatizo linalohusika. Hivyo imembidi kutembelea maeneo mbalimbali ya maktaba kwa ajili

ya kukusanya data za utafiti wake. Maktaba alizotembelea ni halmashauri ya wilaya ya Iramba, Shule ya Sekondari na maktaba ya Mkoa wa Singida.

### **3.7 Uchambuzi wa Data**

Mtafiti ametumia mbinu ya kimaelezo katika kuchambua data za utafiti wake. John (2007) anaeleza kwamba uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kuona au kusoma kazi ya fasihi tamthiliya ikiwemo, kisha kuelewa maudhui ambayo yamebeba dhamira, falsafa, migogoro, ujumbe na mtazamo / msimamo wa mtunzi. Katika kufanya hivyo pia mtafiti ataelewa siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota Tom Mboya*.

Katika kufanikisha uchambuzi wa data katika utafiti wake mtafiti atafanya yafuatayo:-

Kwanza itambidi kusoma kwa kina tamthiliya iliyoteuliwa ili kupata data za utafiti zinazohusu siasa na itikadi. Kila alipopata data husika aliinukuu katika daftari la kukusanyia data na kuzitolea maelezo yanayohusu malengo makuu, yanayojibu maswali ya utafiti wake.

#### **3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo**

Kothari (1990) anaeleza kwamba, mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa kimaelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu. Omari amemnukuu John (1997) kwa kuelezea mkabala wa kimaelezo kwamba ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma shairi, kisha kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo wake na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, mbinu

hii huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo iliwezesha kujibu maswali ya utafiti husika.

Katika utafiti, mkabala huu unamwezesha mtafiti kupata data zilizo katika maelezo kupitia maandishi yaliyoko katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.

### **3.8 Vifaa vya Utafiti**

Vifaa vya utafiti ni jumla ya vitu na zana zote ambazo zitatumika katika zoezi zima la ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti tangu unaanza mpaka mwisho wa utafiti huo. Data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia vifaa mbalimbali vifuatavyo:

#### **3.8.1 Kompyuta**

Kifaa hiki kilitumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti kwa namna mbili. Kwanza kilitumika katika kukusanya data za upili kwa kusoma makala pepe zitakazopatikana katika wavuti na tovuti. Pili, kifaa hiki kilitumika katika kuchapa kazi hii na kuifanya kuonekana vema.

#### **3.8.2 Matini**

Mtafiti ametumia vitabu katika utafiti huu kwa ajili ya kuchunguza na kubainisha masuala ya siasa na itikadi yaliyojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Toma Mboya* aidha vitabu vya uhakiki, magazeti na makala mbalimbali zote zilitoa mchango mkubwa kupatikana kwa data katika kufikia malengo ya utafiti huu.

### **3.8.3 Kalamu**

Kalamu ni kifaa kinachotumika kuandikia. Mtafiti alitumia kalamu ya wino kuandikia kwa kukusanya na kuchambulia data za msingi kwa maana tamthiliya *teule* na zile za upili kutoka maktabani.

### **3.8.4 Shajala**

Ni vifaa kama vile kalamu, karatasi (ream papers), rula na daftari. Vyote hivi vilitumiwa na mtafiti alipokuwa akikusanya na kuchambulia data za msingi kutoka katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* na kunukuu data za upili zilizopatikana katika machapisho na makala mbalimbali.

## **3.9 Usahihi wa Data**

Usahihi wa data, ni utaratibu anatumia mtafiti katika upatikanaji wa data sahihi na za kuaminika (Cohen na wenzake, 2006). Katika upatikanaji wa ukusanyaji wa data sahihi za utafiti wake, mtafiti atatumia maktaba kuchambua data katika tamthiliya husika. Katika uchambuzi huu wa data mtafiti atajikita zaidi katika kuchunguza siasa na itikadi zilizo jitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kwa mbinu ya uchambuzi wa mkabala wa kinadharia na uchambuzi wa kimaelezo.

## **3.10 Maadili ya Utafiti**

Enon (1998) anasema, “Mkabala wa maadili ya utafiti ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, akitekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake” miongoni mwa mambo muhimu ambayo anatakiwa mtafiti kuyazingatia ni kama vile kupata kibali

cha kufanya utafiti, kutunza siri za watafitiwa, kuheshimu mipaka ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data. Katika utafiti wake mtafiti alitakiwa kuzingatia maadili hayo ili aweze kupata data sahihi na muhimu katika kazi yake.

### **3.11 Hitimisho**

Mtafiti amewasilisha mbinu za utafiti ambazo atazitumia katika kukusanya na kuchambua data za utafiti wake, kupitia machapisho yaliyoko maktabani, ambapo mbinu ya maktaba inahusu mtafiti ukusanyaji wake wa data uanze kusoma kwa makini kazi tangulizi zinazohusiana na mada yake ili aweze kupata data za msingi. Data za msingi alizikusanya baada ya kusoma kwa makini tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo.



## **SURA YA NNE**

### **4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza suala la siasa na itikadi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo (2016). Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sura hii ina sehemu tatu, sehemu ya kwanza inahusu siasa katika tamthiliya teule, sehemu ya pili ni itikadi katika tamthiliya na sehemu ya tatu ni uhusiano kati ya siasa na itikadi kisha hitimisho.

#### **4.2 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya (2016)**

##### **4.2.1 Utangulizi**

*Nyota ya Tom Mboya* ni tamthiliya ya Emmanuel Mbogo. Tom Mboya alizaliwa mwaka 1930 nchini Kenya alikuwa mwanasiasa maarufu, Waziri wa uchumi na maendeleo pia alikuwa Mbunge. Kiongozi huyu kijana alikuwa mwenye uwezo, hekima na umahiri katika kupanga mikakati madhubuti iliyolenga kuwapatia maendeleo Wakenya wote. Licha ya mikinzano na hila za kisiasa na kiitikadi, mizengwe na minyukano ya chini kwa chini ya ukabila ifanywa na wapinzani wake pamoja na hujuma hizo bado Tom Mboya alikubalika na makabila yote na alifanikiwa kupata ushindi katika kila uchaguzi, kwa mfano, alishinda ubunge katika jimbo ambalo sehemu kubwa ya wapiga kura hawakuwa watu wa kabila lake. Tom Mboya alifariki akiwa na miaka 39 tu baada ya kupigwa risasi katika mtaa unaoitwa leo *Moi Avenue*.

Hayati Tom Mboya ataendelea kukumbukwa barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla kwa kupigania maendeleo ya watu wake katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kiitikadi bila ubaguzi.

### **4.3 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data**

Uwasilishaji na uchambuzi wa data umejikita katika kuchunguza siasa na itikadi zilizojikeza na kujaiwa katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*.

#### **4.3.1 Siasa na Itikadi katika Tamthiliya Teule**

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ni kubaini siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa njia ya usomaji wa machapisho ambapo mtafiti amesoma, kuchambua na kuchunguza siasa na itikadi katika matini husika. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama yanavyojionesha katika sehemu zinazofuata.

#### **4.3.2 Siasa Katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya**

Katika kuchunguza siasa inayojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, utafiti huu umebaini kuwa msanii anaibua siasa za aina mbalimbali. Kwa hiyo, utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya hiyo inadhihirisha siasa kama vile; siasa na harakati za ujenzi wa jamii mpya, uongozi bora na imani kwa wananchi, ukombozi wa nchi za Afrika, elimu na maendeleo, siasa za ukabila, hofu na tamaa ya madaraka, Kujitoa muhanga, Nafasi ya mwanamke katika siasa, Uhusiano wa nchi za Afrika na zile za magharibi na vibaraka wa kisiasa na umwagaji wa damu.

#### 4.3.2.1 Siasa na Harakati za Ujenzi wa Jamii Mpya

Katika ujenzi wa jamii mpya, Nyerere (1967:6-7) anaona kuwa hatua ya kwanza ni kutoa elimu na watu kujifunza ili kujitambua wao ni akina nani na wanalojukumu gani katika kuleta maendeleo kwa jamii zao. Katika kuonesha umuhimu wa elimu, Nyerere (1973) anadai kwamba, wasomi wanao mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii na anawaomba watumie taaluma zao kwa manufaa ya jamii. Vilevile anaendelea kueleza kuwa, jamii yetu inahitaji wasomi, nakuwa, wasomi wanahitaji jamii. Maneno haya ya mwalimu Nyerere yanatekelezwa kwa vitendo mnamo 1977 katika sera ya elimu kwa wote UPE (Universal Primary Education) ambapo pamoja na mambo mengine ili kusudiwa kwamba nchi itapata wasomi wengi baada ya muda mfupi, ambao wataitumikia nchi na kuleta maendeleo yatakayo wanufaisha wananchi wote.

Fikra hizi nzito za Baba wa Taifa, zinamuingia vema Tom Mboya kwa kuwatafutia ufadhili wa masomo kwa vijana wa Kenya bila kubagua kwamba huyu ni wa rangi gani, wa kabila gani, anatoka kanda gani au dini gani. Hii inadhihirishwa katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* pale Mboya anaposema:

MBOYA: *Safari ilikuwa ndefu. Toka Accra nilitua U.S. Nilifaulu kupata students Airlift Scholarship nafasi 1000. Tengeneza tangazo kisha litume printmedia zote (uk.21).*

Kwa dondoo hii mwandishi amemchora Tom Mboya kuwa aliitumia nafasi yake katika uongozi kutafuta nafasi 1000 kwa ajili ya wanafunzi kwenda kusoma nchini marekani, nafasi hizo hazikuwa za ubaguzi wa kikabila, dini wala tofauti za kiitikadi katika vyama vyao. Suala la usawa katika nafasi hii lilitambuliwa na Wakenya wengi kama Wairimu alivyokuwa anaongea na bosi wake Tom Mboya jinsi kamati

ilivyozingatia fursa sawa kwa kila mtu. Kupitia maelezo ya Mboya na Wairimu wanaongea:

**MBOYA:** *Vizuri. Tunahitaji kuwapa barua na hundi zao Leo Leo Ili waanze matayarisho ya kwenda masomoni, Marekani. Nadhani suala la jinsia Tumelizingatia. Tunao wanawake wakutosha wa MA na PhD (uk.48).*

**WAIRIMU:** *Ni kweli bos. Hata katika suala la fursa sawa kwa makabila yote, Kamati yako ilizingatia maagizo yako (uk.48-49).*

Kwa maelezo haya mwandishi amemtumia *Tom Mboya* kama mwanasiasa mzalendo na mwenye mapenzi mema na watu wake, pamoja na kuwa katika harakati zake za kisiasa lakini bado alipigania ustawi wa watu wa Kenya pasipo ubaguzi wa aina yoyote ile.

#### **4.3.2.2 Uongozi Bora na Imani Kwa wananchi**

Nyerere (1967) anaeleza kuwa, uongozi mzuri ni ule ambao nia yake ni kuwaletea wananchi maendeleo kupitia sera na mipango mizuri. Sera na mipango hiyo mizuri, hutokana na wananchi wenyewe na kazi ya serikali ni kusimamia na kuwezesha wananchi kuandaa sera na mipango mizuri ya maendeleo. Hili litafikiwa kama serikali itakuwa imeandaa namna bora za kuwafanya wananchi wake kuwa weledi katika fani mbalimbali za ustadi katika maisha. Tamthiliya ya Mbogo (2016) Nyota ya Tom Mboya imezungumzia hili. Dhana ya uongozi bora inayorejelea utumishi ambapo serikali iliyoko madarakani inasimamia katiba sio vinginevyo hii ni pamoja na kufuata demokrasia na haki za binadamu. Watu huchaguliwa au kuteuliwa na kupewa dhamana ya kuongoza kwa maana ya kufanya maamuzi na kusimamia maamuzi hayo kwa matakwa ya wale waliowachagua au kuwateua. Mbogo (2016)

*Nyota ya Tom Mboya* anaonesha kuwa, Tom Mboya alipigania maendeleo ya nchi bila upendeleo wowote, hii inajidhihirisha pale Rais Nguruma alipokuwa anamsifia Tom Mboya na kuwaaminisha Wakenya kuwa ni kiongozi bora na makini. Mwandishi anasawiri hali hii kwa kusema: Nimepata habari nzuri juu yako; kuwa : Viongozi wote wa Afrika huko Accra walikuteua wewe kuwa Mwenyekiti wa mkutano? Huku akiwa na furaha, anawaeleza mawaziri, “Kila siku nawaambia Wakenya; *Tom Mboya* ni lulu ya pekee katika chanza ya serikali yangu.”(uk. 16).

Taarifa za Tom Mboya hazikumfikia Rais Nguruma pekee bali waandishi na wananchi wengi nchini Kenya. Tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, inadhihirisha pale mwandishi wa habari Sofia alipo taka ukweli kutoka kwa *Mboya* mwenyewe juu ya suala hilo kwa kuuliza swali: Tunakupongeza, kwani tulizipata habari kuwa Marais wote wa Afrika huko Accra, walikuchagua wewe Mheshimiwa *Tom Mboya* kuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo wa Kihistoria ulioitishwa na Rais Kwame Nkrumah. Hakika umeipa heshima kubwa nchi yetu tukufu ya Kenya (uk.11). Ishara ya wananchi wa Kenya kuwa na imani kubwa na Mheshimiwa Tom Mboya ilianza kujionyesha mapema. Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya* imebainisha umati mkubwa wa wananchi waliojitokeza kumlaki uwanja wa ndege bila kujali tofauti ya itikadi zao aidha ya kikabila, kieneo ama kidini. Kwa kumtumia Omolo mwandishi anasema:

OMOLO: *Tumekuja kumpokea shujaa wetu, Mheshimiwa Tom Mboya. (mapokezi hayo yalianikizwa na wacheza ngoma, Baadhi ya watu walibeba mabango yaliyoandikwa: TOM MBOYA MBUNGE WETU KARIBU, TOM MBOYA CHAGUO LA WAKENYA WOTE ( uk.10).*

Huu ni mfano mzuri kwa wanasiasa na wanaharakati hususani nchini Kenya na Afrika Mashariki kwamba kiongozi bora hujipambanua, mwandishi amemtumia Tom Mboya kama kielelezo cha kiongozi anayependwa na kuaminiwa na wananchi bila kujali tofauti zao.

#### **4.3.2.3 Ukombozi wa Nchi za Afrika**

Mapambano ya kutafuta uhuru wa siasa katika Afrika yameendelea sana toka mwaka 1967. Msumbiji, Angola na Guinea-Bissau sasa hivi ni nchi huru zilizo wanachama wa umoja wa nchi huru za Afrika. Mapambano ya kutafuta uhuru katika Zimbabwe na Namibia, yamesogea mbele sana sasa kuliko yaliyokuwa miaka kumi iliyopita. Yote hayo ni mafanikio ya wananchi wenyewe katika nchi hizo; hakuna mtu mwingine aliyepigania uhuru katika siku za nyuma. Tumeutimiza wajibu huo, na tunaendelea kuutimiza hata leo; hatutabadilisha msimamo wetu. Wala hatutasita kuunga mkono kwa ukamilifu kwa njia ya siasa au ya kibalozi juhudi zote za kupinga ubaguzi wa rangi. Bali tutaendelea na juhudi zetu za kuwatenga makaburu wa Afrika ya kusini kwa njia za utamaduni, uchumi na kisiasa; tutaendelea kutoa kila msaada tutakaoweza kuutoa kwa wale wanaoteswa kutokana na ukatili wa makaburu. Na wala hatutasita kutoa msaada wa kijeshi, kama tukiombwa, kutetea uhuru wa nchi za jirani (Nyerere, 1977).

TUKI (2004) inasema kwamba, ukombozi ni uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu au hali duni. Utafiti huu ulichunguza namna nchi za Afrika zilivyokuwa zinapambana na ukoloni mamboleo, kwani kipindi hiki nchi nyingi za Afrika zilishapata uhuru lakini baadhi ya nchi za Afrika hususani zilioko kusini mwa

Afrika zilikuwa bado zimo kwenye makucha ya mabeberu. Viongozi wa Afrika walipenda bara la Afrika kuungana na kuwa nchi moja. Tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, imezungumzia suala hili pale Tom Mboya Waziri wa Uchumi na maendeleo nchini Kenya na mwenyekiti wa mkutano wa Accra-Ghana ulioitishwa na Rais Kwame Nkrumah alipo ulizwa swali na mwandishi wa habari Sofia na kumjibu kwa kusema: “Huko, viongozi wote wa Afrika kaulimbiu yetu ilikuwa moja : Uhuru wa nchi zetu hautakuwa umekamilika; hautakuwa na maana yoyote, kama nchi nyingine kusini mwa Afrika zitakuwa bado zinatawaliwa na wakoloni, mapambano ya silaha dhidi ya ukoloni na ukaburu huko Msumbiji, Angola, Namibia, Zimbabwe na Afrika ya Kusini ni *Aluta Continua!*.”(uk.11).

Kama haitoshi, viongozi wa Afrika walikutana tena nchini Addis Ababa lengo kubwa lilikuwa ni kuhakikisha Afrika kuungana. Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya* imebainisha hili pale Tom Mboya anapojibu swali baada ya kuulizwa na mwandishi wa habari na kusema:

SOFIA: *Umetuletea nini toka Addis Ababa, Mheshimiwa Tom Mboya?*

MBOYA: *Toka Addis, nimewaletea siasa! Katika mkutano wa Addis Ababa msisitizo ulikuwa: Afrika lazima iungane. Iwe na Serikali moja, Rais mmoja, kabeneti moja, Bunge moja!*

SOFIA: *Manshallah! Hilo linawezekana kweli?.*

MBOYA: *Hili linawezekana iwapo marais wote wakidhamiria (uk.65).*

Kila wanapokutana waungwana kwa lengo la kufanikisha mipango yao, huwa hapakosi misugvano baina yao, lakini mwisho wa siku hutatua tatizo na kufikia

muhafaka. Katika mkutano wa Addis Ababa, Rais Kwame Nkrumah wa Ghana na Rais Julius Nyerere wa Tanzania, walitofautiana sana kwaajili ya mustakabali wa vipi muungano wa Afrika unaweza kupatikana? Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, imebainisha jinsi magwiji wa siasa barani Afrika walivyo charurana juu ya suala hili, haikuwa kwa nia mbaya wala uhasama la hasha bali kulikomboa bara la Afrika. Mwandishi anabainisha hili kupitia mahojiano ya Tom Mboya (mwanasiasa) na Sofia (mwandishi wa habari).

*SOFIA: Mheshimiwa Tom Mboya; taarifa tulizozipata ni kuwa Rais Kwame Nkrumah na Rais Julius Nyerere wa Tanzania, walikwaruzana sana Kuhusu mustakabali wa vipi muungano wa Afrika unaweza kupatika Ebu tufafanulie kidogo juu ya hili!*

*MBOYA: Ni kweli majabali hawa wawili wa siasa za Afrika walikwaruzana. Lakini hatimaye, tulifaulu kuwapatanisha.*

*SOFIA: Sasa walikwaruzana na kuhitilafiana katika lipi hasa?*

*MBOYA: Eeh... Osagyefo Kwame Nkruma anashikilia kuwa: Afrika iungane yote kwa pamoja. Mara moja. Kwa wakati mmoja. Lakini Rais Nyerere anasema. Hapana. Anasema nchi za Afrika zinaweza kuungana kwa kanda. Sasa, hapo ukalipuka mdahalo mkali sana. Lakini, Kama nilivyoeleza, hili, hatimaye tulilimaliza vizuri (uk.65-66).*

Kutokana na maelezo haya inaonyesha jinsi viongozi wa Afrika walivyopambana na kupigania ukombozi wa bara la Afrika, hivyo mbinu mbalimbali zilitolewa kulikwamua bara la Afrika mikononi mwa mabeberu. Rais Nkrumah wa Ghana na JK Nyerere walikuwa mfano wa viongozi wazalendo.

#### **4.3.2.4 Elimu na Maendeleo**

Elimu ni chombo muhimu kwa maendeleo. Hivyo mzazi awapeleke watoto shule na pia ajielimishe yeye mwenyewe. Atumie njia mbalimbali katika kujiendeleza. Kwa



mfano kusoma vitabu, magazeti, kusikiliza radio na ushiriki katika ELIMU YA WATU WAZIMA (WET, 1974). Maendeleo ya nchi huletwa na watu, hayaletwi na fedha. Fedha ni matokeo siyo msingi wa maendeleo. Ili tuendeleo twahitaji vitu vinne: Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora (Nyerere, 1969).

Mtafiti alibaini kuwa siasa ilianikiza suala la elimu na maendeleo katika nchi ya Kenya. Tunamuona mwandishi Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amebainisha kuwa chachu ya maendeleo ni elimu jamii isiyokuwa na elimu inaishia kwenye matatizo makubwa. Hili linajitokeza pale uwanja wa ndege umati wa watu ulipojitokeza kumpokea mwanasiasa Tom Mboya, na kumuuliza swali, nini mustakabali wa nchi ya Kenya mintarafu uchumi na maendeleo?. Swali lilijibiwa na mwanasiasa *Tom Mboya* kwa kusema:

*MBOYA: Swali zuri. Kwanza: jabali la maendeleo ni elimu. Dira ya maendeleo katika jamii ni elimu. Ujinga ni utasa, ni jangwa. Bali elimu huzaa maafa, ujuzi na stadi mbalimbali. Hata tuwe na itikadi zilizo takata kiasi gani; bila elimu madhubuti ni sawa na waogeleaji vipofu wanaojaribu kuokoa maisha yao katikati ya bahari mchafukoge. Elimu ni ufunguo wenye uwezo wa Kufungua makufuli na minyororo yote ya umaskini. Huu si msemu chakavu, aslani. Nchi isiyotoa elimu madhubuti vijana wake watakuwa sawa na tai aliyepunyuliwa manyoya yote akabaki uchi. Ataruka? Hawezi. Programu ya Students Airlift niliyoianzisha miaka ya nyuma, kwa mfano, ni ushahidi na udhibitisho wa lile ninaloliamini na kulipigania. Na kwa taarifa ni kuwa: Marekani wamenipa Scholarship nyingine 1,000 katika mpango huu wa Airlift kwaajili ya vijana wetu (uk.11-12).*

Kwa nukuu hii, taifa lenye watu wasio na elimu ni vigumu kupata maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla. Tom Mboya aliliona hili mapema, pamoja na harakati zake za kisiasa aliweza kupambana hadi akapata scholarship 1000 kwa wanafunzi wa Kenya kwenda Marekani kupata elimu ambayo itakuwa mkombozi katika nchi yao.

Mwalimu Julius K. Nyerere wa Tanzania alisisitiza kwa kusema, taifa lipate maendeleo sharti watu wake wapatiwe elimu kwa kufuta ujinga.

#### 4.3.2.5 Siasa za Ukabila

Katika uchunguzi wake, mtafiti alibaini tatizo la ukabila lilitamalaki katika siasa za Kenya, mwandishi Mbogo katika tamthiliya yake ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) amelielezea hili kwa mfano *Obama Sr* alivyokuwa anaongea na *Tom Mboya*.

OBAMA Sr: *Juzi nilikuwa Kisumu. Ker Omondi aliitisha mkutano. Unajua Omondi hakutaki wewe. Anamtaka Owino Okaka apiganie ubunge wa Jimbo la Nairobi. Anakuona wewe kama: you are not pure Luo! (yaani sio mjaluo halisi) naye Mboya alijibu kwa maskhara (uk. 25)*

MBOYA: *Ni chotara: Tom ni chotara! Mchanganyiko wa Jaluo, Kamba, Kikuyu, Kalenjini, Kisii na.....?(uk.25)*

OBAMA Sr: *Na Maasai!(uk.25)*

Pamoja na Ker Omondi kufanya siasa za ubaguzi wa kikabila bado wananchi wa Kenya walimpenda Tom Mboya kama mkombozi wao, mtafiti alilibaini hili kupitia tamthiliya ya Mbogo (2016) Tom Mboya.

MBOYA: *Tazama juzi Airport?(uk.25)*

OBAMA Sr: *Umati. Makabila yote yalimiminika kuja kukulaki (uk.25).*

MBOYA: *Nakuambia Obama, huu ukabila tukiendelea kuupakata na kuulea, huko mbele itakuwa shida (uk.25).*

Kwa nchi ya Tanzania, suala la ukabila lilizikwa mapema na aliyekuwa Rais wa Tanzania hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kitendo hiki kiliwavutia nchi mbalimbali ikiwemo Kenya. Kwa mfano, Mboya anamwambia Obama, “ *I, think we need to borrow a leaf from Mwalimu Nyerere.*

OBAMA Sr: *Yah. Katika hili, Nyerere anaelekea kufanikiwa (uk.25).*

Mbongo (2016) mwandishi wa tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, amemchora mwanasiasa na Waziri wa Uchumi na Maendeleo wa Kenya, Tom Mboya alikuwa na ndoto ya kuwa Rais wa Kenya ili aweze kuung'oa ukabila, kwa kinywa chake mwenyewe Tom anasema:

**MBOYA:** *Basi ndoto ya Martin Luther King ni ndoto yangu. Natamani nije niingie Ikulu ili tuweke msingi wa kuung'oa ukabila na kuleta maendeleo kwa wote (uk.36).*

Tom Mboya anaanza Kuihutubia hadhira.

*Ndugu Wakenya wenzangu,  
Ninayo ndoto!  
Kuwa watoto wetu  
Hawatapimwa katika mizani ya ukabila  
Bali watatathiminiwa kwa uwezo wao  
Watahukumiwa kwa wema ama ubaya wao  
Wala si kwa makabila au dini zao!  
Watoto wote wa Kenya  
Watoto wa makabila yote  
Watasoma pamoja  
Watakula pamoja  
Watakumbatiana pamoja  
Wavulana watawabusu wasichana wa makabila yote!  
Na wasichana watawakumbatia wavulana wawapendao.  
Watafunga ndoa za mapenzi  
Sio ndoa za: “wewe kabila gani?”  
Ama: “wewe wa dini gani?”  
Watoto watakuwa Taifa moja  
Na nuru ya Kenya itaangaza duniani kote  
Ninaota!( uk.36-37).*

Kauli hii ni mfano mzuri kwa nchi na jamii zinazoendekeza ubaguzi wa aina mbalimbali kama vile; ubaguzi wa kabila, rangi, dini, siasa na itikadi tofauti kupiga vita suala hili. Tom Mboya alikuwa na ndoto siku atakapoingia ikulu atahakikisha anawaunganisha Wakenya wote kwa kujenga misingi ya umoja na kuondoa ubaguzi wa aina yoyote na kuwaletea maendeleo watu wote kwa wananchi kuzalisha mali kwa kushirikiana.

#### 4.3.2.6 Hofu na Tamaa ya Madaraka

Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, mtafiti ailibainisha kuwepo kwa wanasiasa wenye tamaa ya madaraka na hofu ya kukosa urais. Mwandishi amewachora wanasiasa Tuta, Kanoga na Chega jinsi walivyo jawa na tamaa ya madaraka hususani ngazi ya juu katika nchi ya Kenya kama walivyokuwa wanajadiliana:

CHEGA: *Tom Mboya ndiyo ishuh!* (uk.40)

TUTA: *Enh! The guy is just too shrewd. Hana ujadhe sana. Karibu makabila yote nchini yanamkubali. Ukitokea uchaguzi aidha bungeni ama nchi nzima hakuna atakayeweza kushindana na Tom Mboya* (uk. 40).

KANOGA: *Hata watu wetu watampigia kura. Hiki ni kitendawili* (uk.41).

TUTA: *Kama Mzee ...Well...Hatuombe; na Mungu apishilie mbali: Kama mzee akiondoka ghafla. Tom Mboya anaweza akachukua Urais wa Kenya* (uk.40- 41).

Maelezo haya yanathibitisha kuwepo kwa itikadi za kisiasa zilizojaa ukabila katika nchi mbalimbali mfano Kenya, baadhi ya wanasiasa waliendesha kampeni zao kwa kufuata mlengo wa kikabila lakini wanasiasa wengine walijawa na uroho wa madaraka, kwa mfano Tuta, Chega na Kanoga walikuwa na hofu kwamba, siku moja Tom Mboya angeweza kuwa Rais wa Kenya kutokana na kupendwa na wananchi wa Kenya bila kujali itikadi zao kutokana na hali hiyo wanasiasa hawa walifika mbali kiasi cha kutaka kuifanyia marekebisho katiba ya nchi. Mtafiti alilibaini hili katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, Chega na wenzake wakiwa kwenye mkutano mkali Tuta akiwa mwanzilishi:

TUTA: *Kanoga, tunahitaji kuifanyia katiba marekebisho haraka iwezekanavyo. Endapo uking'oka mbuyu; sharti upandwe mbuyu pahala pake* (uk.14).

CHEGA: *Lakini kama katiba itabaki ilivyo, hata michongoma inaweza kupandwa mahali pa mbuyu (uk.14).*

TUTA: *Sikilizeni mtu hatari kuliko wote ni Tom, siyo Omondi wala Abdalla. Tukizembea, Tom Mboya atarithi kiti cha Nguruma. Kama nilivyoeleza awali: Tunahitaji kurekebisha vifungu kadhaa vya katiba ili kumbana Tom. To be honest that man is so intelligent, smart and articulate kiasi kwamba unapokuwa karibu naye anakufanya u-feel uncomfortable (uk. 14-15).*

Harakati za kufanya marekebisho ya katiba, ilikuwa ni hofu kubwa waliokuwanao wanasiasa hawa, walimuogopa sana Tom Mboya kwa kukubalika na makabila yote, kauli hii inadhihirishwa na Tuta anaposema:

TUTA: *Tatizo ni kwamba hata katika suala la ubunge, makabila yote ya Nairobi humpigia kura Tom Mboya. I don't know whats wrong with our people (uk.15).*

Wanasiasa hawa walikosa ubinadamu kabisa pale walipokutana ikulu kwa ajili ya mkutano ambao ulihusu hali ya Mtukufu Rais Nguruma na kifo cha mwanasiasa Abdulla. Tuta alitaka suala la katiba liangaliwe, alianza kusema:

TUTA: *Mheshimiwa Mwenyekiti; Kama afya ya Mtukufu Rais bado ni tete na tata; basi naona kuna haja ya kuingalia katiba ili kuifanyia marekebisho. Mwandishi amemchora Tom Mboya alivyosikitishwa na kauli ya Tuta kwa kutoa angalizo (uk.29).*

TUTA: *Na ni afadhali achukue Urais mtu yeyote lakini siyo TM. Huyu Ker Omondi tutamweka ndani; lakini kuhusu TM, tunahitaji tufanye uamuzi mgumu (uk.41).*

MBOYA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha. Ni jambo lakushangaza kuwa: mwanasiasa maarufu; colleague na mwanaharakati mwenzetu, kauwawa jana. Maiti yake ipo mwochware ndani ya jokovu baridi. Yaani ni kweli roho zetu zimezizima kama mwili wa Abdalla huko uliko? Yaani hatuwezi, hata Kama Ni kiitifaki tu; tukaanza mkutano huu Kwa ukimya, Na Kama matawi ya mforosadi, tukainamisha vichwa vyetu Kwa huzuni, Kwa sekunde*

*moja, tukaomboleza pamoja na mjane Yasimin na binti yao Zera?  
Kipaumbele si kurekebisha katiba; kipaumbele si siasa na itikadi.  
Kipaumbele ni ubinadamu (uk.29-30).*

Kwa maelezo ya Tom Mboya yanathibitisha kuwa wanadamu hususani wanasiasa wanaotafuta madaraka kwa nguvu hawana ubinadamu kabisa. Kwa mfano Tuta na wenzake walitaka suala la mabadiliko ya katiba ya nchi lifanyiwe mabadiliko, lengo lao hofu ya kuukosa Urais endapo Mzee Nguruma angefariki dunia baada ya kuandamwa na maradhi.

#### **4.3.2.7 Kujitua Muhanga**

Katika uchunguzi wake mtafiti alibaini wananchi na wanasiasa nchini Kenya waliweza kujitua muhanga katika kupigania uhuru wao, katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, Tuta, Kanoga na Chega wamechorwa wakilijadili katika ukumbi wa mikutano ikulu:

**KANOGA:** *Inatubidi tujipange kabla ya mkutano na Rais. Watu walijitua muhanga. Watu walitua sadaka kwa uhai wa damu iliyomwagika walipochinjwa kama mbuzi. Damu yao ikawa kafara kwa ajili ya nchi hii. Ardhi nayo ikaachama na kuinywa damu hiyo kama hijabu ya madonda yalitokana na mtutu wa bunduki ya mkoloni. Na kweli, leo majeraha, ngeu na vilema vilivyotokana na vita vya maumau ndiyo kwanza yanaanza kupata afueni (uk.14).*

Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amemchora Omondi jinsi alivyojitua muhanga kwa kuwakoromea wakoloni ili waweze kumfungulia Nguruma kwa kusema:

**OMONDI:** *Ama kweli fadhila za punda, mateke. Wakati ule, niliwakoromea wakoloni, nikawaambia: “Nguruma ni mungu wa Wakenya wote. Mfungulieni Nguruma, ndipo Kenya ipewe uhuru.” Lakini sasa najua nilikulisha adesi bwana Nguruma (uk.18-19).*

Baada ya wanasiasa maarufu kuhitilafiana na uongozi wa wajuu, walianza kutafuta njia mbalimbali ya kushika dola, kwa mfano Ker Omondi kujitoa kwenye chama tawala na kusajili chama cha upinzani. Mwandishi amelibainisha hili kwa kumchora Obama Sr kwa kusema:

OBAMA Sr: *Ker Omondi amesajili chama cha upinzani (uk.35)*

MBOYA: *Hawa jamaa wanataka kutusambaratisha. Wanakula njama ya kuitema, kuiangusha na kuitia moto nguzo ya umoja wetu? Tunahitaji kufanya jambo (uk.35).*

Hapa inaoneshwa kuwa, umoja ukilegalega mipango yote mizuri huvurugika na kuyeyuka, methali ya Kiswahili inasema umoja ni nguvu na utengano dhaifu. Ker Omondi na mwenzake Abdulla walipigania kujenga uchumi wa nchi kwa misingi ya itikadi ya kijamaa lakini wanaharakani wengine hawakukubaliana na itikadi hiyo. Kutokana na utofauti huo makundi yalizuka miongoni mwao na uadui ulianza ambapo makundi haya yalishirikiana na washirika wao nje ya Kenya kuhakikisha wanashika dola hata kwa kumwaga damu, hili limeshuhudiwa mauaji yaliyofanywa na vibaraka kama vile; Zolo na Jackal wakifadhiliwa na CIA walivyomuua Abdulla. Duma na Chatu kumuua Tom Mboya wakiwa wametumwa na KGB.

#### **4.3.2.8 Nafasi ya Mwanamke Katika Siasa**

Wanawake wa Afrika wamekwisha kujionyesha kuwa ni wa maana sana katika vita vya kimapinduzi. Walitoa msaada wao madhubuti katika vita vya kupigania uhuru katika nchi mbalimbali na katika hali nyingine, na kushiriki kwao kwa kijasiri katika maandamano na aina nyingine za vitendo vya kisiasa, kulileta matokeo ya uamuzi. Kwa hiyo wanayo rekodi nzuri ya kimapinduzi na ni chanzo kikubwa cha nguvu kwa

vyama vyetu vya kisiasa na vita. Uwezo wao na ufundi wao lazima utumiwe hadi kufikia kikomo (Chiume, 1980: 55).

Katika utafiti wake, mtafiti alibaini kuwepo kwa mchango katika harakati za siasa na ni muhimili wa maendeleo katika familia na Taifa kwa ujumla, tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, anabainisha kauli hii kwa kumwelezea Pamela ( Mke wa Tom Mboya) kuhusu mumewe na siasa. Pamela alitamani mumewe aachane na siasa kwani aliona mumewe anatumia muda mwingi kwenye siasa badala kuwa karibu na mkewe. Pamela anasema:

PEMELA: *Nasema: Natamani ningekuwa na uwezo; ningekuwa na ujasiri wa kumwamuru Tom ampe talaka huyu mwanamke anayeitwa; siasa. Aoe mrembo aitwae, kwa mfano: The Rusinga Fishing Company. Lakini siasa! Kila kukicha siasa. Ukilala siasa (uk.34).*

Kadri siku zilivyosonga mbele, Pamela alianza kuyazoea maisha ya siasa. Pamela alimtia nguvu mumewe kuendelea na harakati zake za siasa na kuahidi atakuwa na bwanake bega kwa bega katika harakati hizo. Hili linabainishwa na mwandishi wa tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, anaposema:

PAMELA: *Endelea kumkumbatia huyu mke mwenza. Nami nipo pamoja nawe kwa mvua, kwa jua, Hadi mwisho wa dunia (uk.38).*

Pamoja na kuyazoea maisha ya kisiasa, Pamela alikuwa anakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile upweke na uhai na usalama wa mumewe kama anavyojibu swali baada ya kuulizwa na mwandishi wa habari (Sofia).

SOFIA: *Bibi Pamela Mboya; unaweza kutudokezea; unapata changamoto za aina gani kama mke wa mwanasiasa mashuhuri, kama Mheshimiwa Tom Mboya? (uk.66).*



PAMELA: *Changamoto zipo. Tena nyingi. Lakini sasa nimezoea.*  
 PAMELA: *Kwanza upweke anapokuwa safarini.*  
 PAMELA: *Ya pili ni uhai wake. Uhai na Usalama wa Tom. Wakati mwingine nahofia maisha yake. Wakati mwingine nahisi labda nyota hii itazimika kabla ya wakati. Lakini kwa vyovyote vile, nadhani jambo kubwa ni Kumwomba na kumtegemea Mungu (uk.66).*

Mwanamke anayo nafasi kubwa katika ujenzi wa taifa lake pia ni mwaminifu katika usimamizi wa majukumu aliyokabidhiwa vilevile ni watu wenye huruma sana. Kwa mfano, Pamela alikuwa anahofia uhai wa mme wake Tom Mboya hususani alipokuwa ziarani nje ya nchi ya Kenya aidha upweke ulikuwa unamsumbua sana. Hata hivyo alimtia shime bwanake aendelee katika harakati zake za kisiasa kuipigania Kenya iweze kujikomboa kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kifikra.

#### **4.3.2.9 Uhusiano wa Nchi za Afrika na zile za Magharibi**

Ushirikiano wa Afrika Mashariki unahitajiwa na bara zima; ushirikiano wetu umekuwa, na unaweza ukawa tena, silaha kubwa katika vita vyetu vya kutafuta maendeleo na uhuru wa kiuchumi. Safari ya kuikomboa Afrika bado ni ndefu (Nyerere, 1977).

Uhusiano baina ya nchi na nchi ni ile hali ya kuwa na mfungamano mzuri au mbaya. Katika utafiti wake, mtafiti alichunguza tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya* na kubaini kuwepo kwa siasa zilizohusu uhusiano wa nchi na nchi. Mwandishi amemchora Tom Mboya jinsi alivyo shikamana na nchi ya Marekani kupitia shirika lake la CIA, aidha ukweli wa kauli hii unathibitishwa na Wanjiru, Tuta, Chega na Kanoga:

WANJIRU: *Lakini si mnajua pia kuwa Tom Mboya ni kipenzi cha CIA (uk.41).*

TUTA: *Sawa kabisa. Na baya zaidi ni kuwa: CIA inafanya juhudi za ziada kung'oa Mzee Nguruma ili Tom awe Rais. Sasa hivi Mboya ana global-trot kwa pesa ya CIA jet set. We have to do something before it too lat (uk.41).*

Mwandishi amemchora Rais Nguruma kuwa ni mshirika wa karibu na Moscow, Urusi. Chega anadhihirisha kauli hii aliposema:

CHEGA: *CIA hawamwamini sana Mzee Nguruma kwa sababu huko nyuma aliwahi kusoma Moscow.*

WANJIRU: *Akabwia bwibwi la Marxism?!*  
Urafiki wa Tom Mboya na CIA ulisababisha Kanoga, Chega na Tuta kuwa na wasiwasi mkubwa kwamba, CIA wanaweza kumuondoa Rais aliyoko madarakani na kumsimika mtu wamtakae ambaye ni Tom Mboya. Kanoga na Tuta wanajadiliana hili:

KANOGA: *Na CIA ni zimwi toka kuzimuni, lenye uwezo wa kumngo'oa Rais mmoja na kumsimika Rais wanayemtaka, popote duniani. Tazama Kongo, kwa mfano. Wamemuua Lumumba na kumsimika kikaragosi Mobutu Seseseko kuku wa Zabanga.*

TUTA: *Na tukichelewa; kwa mabavu na makucha ya mtandao wao, CIA wanaweza Kutuvuruga. Twache joto la Mgoa lishuke miongoni mwa wananchi (uk.42).*

Aidha mwandishi amebainisha kuwepo kwa mahusiano kati ya Abdulla na washiriki wake KGB na Bejini kwani aliwafanyia Warusi kazi nzuri kule Msumbiji. Haya yanaelezwa na chega alipokuwa anaongea na rafiki zake kwa kusema:

CHEGA: *Ndiyo maana safari zake za Tanzania, Msumbiji na Angola zilikuwa haziishi (uk. 40).*

Mazungumzo haya yanaonesha ni jinsi gani viongozi wengi hujiegemeza kwa mataifa yenye nguvu kiuchumi ili waweze kupata misaada na kufikia malengo yao. Mfano mzuri ni viongozi wengi barani Afrika wamekuwa na tabia hii, pindi wanaposhindwa kutekeleza matakwa ya mabeberu huliingiza taifa katika hatari na kuwaumiza wananchi. Haizuiwi kuwa na marafiki isipokuwa uwe na rafiki mwenye nia njema na taifa sio urafiki wa masharti magumu, Tanzania inaamini katika siasa ya kutofungamana na upande wowote, hivyo haibagui. Nchini Kenya wanaharakati wa kisiasa, walikuwa na marafiki wao kama vile; Marekani (CIA) ambapo waliamini itikadi ya kibepari, Urusi na China (KGB) ambapo waliamini maendeleo ya nchi yatapatikana kupitia uchumi wa kijamaa.

#### **4.3.2.10 Vibaraka wa Kisiasa na Umwagaji Damu**

Kibaraka ni kiongozi wa serikali ya taifa uhuru anayetumiwa na serikali za kibeberu kwa faida yao au kiongozi apataye cheo chake kwa msaada wa serikali za kibeberu (TUKI, 2004). Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) Nyota ya Tom Mboya, imewachora viongozi wa kiafrika wanavyo jenga urafiki na mabeberu kwa lengo la kupata misaada ya kisiasa na kiuchumi hususani kushika dola (Urais), kwa hali hii kila mwanasiasa na kikundi chake hujitahidi kupata washirika wenye nguvu lakini matokeo yake ni mauji na ulipizaji visasi kwa mfano Abdulla aliuwawa kwa kupigwa risasi na majambazi Zolo na Jackal kwa kutumiwa na mabeberu naye Tom Mboya aliuwawa kwa kupigwa risasi. Mtafiti alilibaini hili kupitia mazungumzo kati ya Kanoga, Tuta, Wanjiru na Chega:

KANOGA: *Na KGB na Bejini bado wamevaa majoho meusi wakiomboleza. Abdulla alikuwa kuwadi muhimu wa kueneza itikadi za Kimarx. Aliwafanyia Warusi kazi nzuri kule Msumbiji (uk.40).*

WANJIRU: *Na hili ndilo lililochochea hasira za CIA (uk.40).*

WANJIRU: *Na wakati Abdulla akiruka angani, Setlite za Marekani zimekuwa zinanasa na kuhifadhi ujasusi wake wote (uk. 40).*

Mwandishi wa tamthiliya ya *Tom Mboya* (2016) amewachora Duma na Chatu kama watu hatari wauwaji wanatumiwa na vibaraka kumuua *Tom Mboya* na kuizima nyota yake iliyong'aa. Duma na Chatu wanapanga jinsi ya kumuua Tom Mboya.

DUMA: *Kifo cha huyu mtu...du! Nasikia uchungu. Woga. Nawaza pia juu ya mke na watoto wake. Zaidi ya hapo; watu wengi wanampenda. Ni mwanasiasa mahiri kabisa (uk.62).*

CHATU: *Woga ukizidi; ukipaniki tu, utakosea shabaha. Na ukishindwa kumuua; KGB hawatakusamehe (uk.62).*

DUMA: *(anasimama, anachukua 50,000/=) Eifu hamsini (uk.62).*

CHATU: *Duu! Hii inatoshwa kabisa. (Anaziweka mfukoni) (uk.62)*

DUMA: *Wachina na Warusi hao. Wamenipa pesa nzuri (uk.62).*

CHATU: *Nasikia Wachina na Warusi hawamtaki Mboya kwa sababu ya siasa zake za CIA (uk.62).*

DUMA: *Ok. Huyu marehemu mtarajiwa, atarudi leo kwa ndege toka Addis Ababa.Sasa hivi twende Airport. Akitua tu; tutamfuatilia hadi tuitoe roho yake (uk.63).*

Mwandishi ametoa mfano huu sahihi kabisa, viongozi wengi wa kisiasa wamekuwa na siasa zilizojaa fitina na uadui mkubwa lengo ni kushika dola. Mara nyingi yule mwenye nguvu na kupendeka kwa wananchi huandamwa na mikasa mbalimbali iwe kuchafuliwa ama kuuwawa, mambo kama haya yanapojitokeza wanasiasa hawa huanza kusalitiana na kulipizana visasi. Mwandishi amewatumia majambazi Duma

na Chatu kwa kuwapatiwa Tsh. 50,000= kutoka kwa vibaraka wa Wachina na Warusi ili wakamuue Tom Mboya kwa kuhofia angeweza kusimikwa Urais wa Kenya lengo la kumuua lilitiamia ila nafasi waliokuwa wanaitamani hawakuweza kuipata.

#### **4.4 Hitimisho la Mjadala**

Mjadala uliofanyika baada ya uchambuzi wa masuala ya kisiasa katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya* unachangia kwa kiasi kikubwa katika kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu. Lengo letu la kwanza katika utafiti huu lilikuwa ni Kuelezea siasa zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016). Ni dhahiri katika siasa zilizowasilishwa katika sura hii pamoja na mijadala yote, mwandishi anaamini kwamba, siasa nchini Kenya zilikuwa zimejaa changamoto nyingi kama vile; siasa za chuki, fitina, ubaguzi wa kikabila, mikinzano ya kiitikadi na umwagaji wa damu kwa watu wasio na hatia. Kwa mujibu wa Mbogo, ukweli huu umesababishwa na uwepo wa viongozi vibaraka waliojaa ubinafsi na tamaa ya madaraka.

#### **4.5 Itikadi katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya**

Moja ya malengo mahususi ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha itikadi zinazojitokeza katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*. Mtafiti alitumia tamthiliya teule katika uchambuzi wa data zilizohusu itikadi ili kufikia malengo ya utafiti huu, ambavyo ni tamathali za semi na si vipengele vyote vya lugha katika mtindo. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji wa machapisho

kusoma na kuchambua tamthiliya hiyo ili kuweza kubaini masuala ya itikadi yaliyojitokeza katika tamthiliya hiyo.

Aidha data kutoka katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya* zilitumika ili kujaziliza data zilizopatikana katika mapitio ya maandiko.

#### 4.5.1 Itikadi ya Ushirikina

Itikadi ni imani au mtazamo alionao mtu kuhusu maisha kwa ujumla wake, hususani katika kufanikiwa ama kutofanikiwa katika maisha (Chuachua, 2011). Katika utafiti huu alibaini kuwa Mbogo (2016) mwandishi wa tamthiliya ya *nyota ya Tom Mboya* anaibua itikadi ya ushirikina kupitia Nabii alipokuwa anawaagua Kanoga, Tuta, Chega na Wanjiru kwa kuwaelekeza na kutoa masharti ili wasidhurike.

NABII: *Damu ya msichana bikira. Unajua, Iluminata na Baali huwa wawili huwa hawali nyama. Wao hufurahia mvinyo wa damu ya mabikira (uk.53).*

Nabii alitumia maji kama ramri ya kuona mambo mambaya yatakayoweza kuwadhuru akina Kanoga pale aliposema:

NABII: *Naona kitu kama jeneza (uk.54).*

CHEGA: *Jeneza, Mtume, Nabii?(uk.54)*

NABII: *Jeneza linaelea hewani.*

*Wamevaa nguo nyeusi na makoti ya magunia.*

*Waombolezaji wamejipaka tope na majivu.*

*Waombolezaji wanalia na kutapatapa,*

*Wanaimba, wanacheka na kucheza ngoma (uk.54)*

Nabii alipoendelea kuangalia maji aliibuka na kuwaeleza wagangwaji kwamba anaona fujo.

NABII: *Fujo. Naona mbweha kichaa, wenye meno makali wakiushambulia umati wa waombolezaji. Lakini, ajabu kabisa; kwani: naona nao waombolezaji wanachukua matone ya machozi yao toka machoni mwao; na kwa silaha hizi wanawashambulia hawa mbweha kichaa wenye meno mkali. Ajabu kabisa!( uk.55)*

Kanoga, Tuta na Chega walikuwa na shauku ya kuona kile kinachojitokeza kwenye maji lakini Nabii aliwazuia kuangalia.

NABII: *Naona maajabu ya musa: Jeneza limeota mbawa. Jeneza limewaponyoka waombolezaji. Kwa mbawa imara Kama za Tai, jeneza linapaa! Watu wanalia, watu wanashangaa (uk.55).*

Baada ya kuwaaminisha Kanoga, Tuta na Chega, Nabii aliwataka awapatie kinga la sivyo watakufa. Pale anaposema:

NABII: *Na ninyi nyote mtahitaji kinga. La sivyo maji yatawameza na kuwazika chini ya vilindi vya bahari ya Hindi (uk.55).*

Kanoga na wenzake walikubali kupatiwa kinga, zaidi walimshukuru Nabii. Nabii akatoa maelekezo kwa kusema:

NABII: *Kila mmoja atachanjwa chale mbili za pweza usoni. Chale mbili za kinyonga Ubavuni. Chale mbili za bundi utosini. Na wote mtabwia bwibwi la mavumba ya mtoto mchanga. Wewe! Wewe! Na wewe! Hili bwibwi la Iluminata lina pawa ya ulumbi katika hotuba. Jukwaani, hakuna mwanasiasa yeyote atakayefua dafu. Kila uchaguzi wewe utakuwa mshindi (uk.56)*

Katika suala la ushirikina katika maisha ya mwanadamu linajitokeza kama desturi za kidini ambazo zinafuatwa na kuaminiwa na watu kama msingi wa utatuzi wa matatizo yao ambapo suala la dini halizingatiwi kabisa. Dini mbalimbali linachukulia ushirikina kama dhambi kwa kuwa unaashiria utovu wa uaminifu mbele ya Mungu.

Hii inatia nguvu tabia ya ushirikina kwa binadamu kwa sababu mtu anaona kwamba, kwa kufikia hatua hii, usaidizi utafanyika.

#### 4.5.2 Itikadi ya Mapinduzi

Marx (1859) anaeleza kuwa mapinduzi ni hatua muhimu ya kusaidia jamii kupata maendeleo kwa watu wa tabaka la chini kuwaondoa mamlakani watu wa tabaka la juu na kuifanya jamii kuwa haina matabaka. Itikadi ya kimapinduzi haikani tu. Siyo kukanusha kimawazo kanuni za kijamii inayotoweka, lakini ni mawazo yanayojenga, mwangaza unaoongoza hali ya kijamii inayochipuka. Mapinduzi huletwa na watu ambao hufikiri kama watu wa vitendo na wanafanya vitendo kama watu wenye fikra (Chiume, 1980).

Tabaka la juu ni lile linalokaliwa na viongozi ambao hunyonya rasilimali za taifa kwa masilahi yao binafsi na kuiacha jamii ikiwa katika hali mbaya ya umaskini (Bell, 1977). Tabaka hili la juu ndilo linalofahamika kama tabaka la mabepari ambao kazi yao kubwa ni kujilimbikizia mali kutokana na unyonyaji wa rasilimali na nguvu kazi za wanajamii. Mapinduzi ya kuondoa mfumo wa Kipebari ni muhimu yafanyike na kuwezesha kusimikwa kwa mfumo wa Kijamaa ambao utakuwa hauna matabaka baina ya walionacho na wasionacho (Engles, 1892).

katika tamthiliya ya Mbogo(2016) *Nyota ya Tom Mboya*, mwandishi amemtumia Rais Nguruma kama kiongozi asiyesikiliza hoja kutoka kwa watu wengine (viongozi) walio chini yake. Suala hili lilichukuliwa na wanasiasa wawili Abdalla na Omondi ni hali ya ukandimizwaji na kupokonywa haki yao ya msingi wa kutoa maoni.

OMONDI: *Ndugu Rais Nguruma, muarubaini wa maendeleo yetu ni kujenga uchumi wa kijamaa. Ubepari ni subiani atakaye wanyoya damu*



*wananchi. Ubepari ni koleo itakayowaziaka wakulima na wafanyakazi kaburini (uk.17).*

Maelezo hayo yalimchefua sana Rais Nguruma, kwa hasira aliongea mbele ya mawaziri kuonyesha hisia zake:

**NGURUMA:** *Ninyi watu! Mnataka ngoma za masikio yangu zipasuke kwa mirindimo ya ngoma za ukoministi? Mnataka mboni za macho yangu ziingie upofukwa moshi wa itikadi za ukomunisti? Mnataka damu mwilini mwangu isite kutiririka kwa sababu ya sumu ya moma wa ukomunisti? Mnatakaakili zangu ziote magugu ya wazimu kwa sababu ya nyimbo za mahepeya ukoministi? Shetani wa magharibi tunamjua; shetani wa kikomonisti hakuna Mkenya anayemjua ila Mheshimiwa Omondi na Abdalla! Kila kukicha mmeendelea kuwa mwiba katika serikali yangu. Nimechoka! (uk.18).*

Tofauti za kiitikadi baina ya viongozi hawa wawili na Rais Nguruma hazikuvumilika kwa Omondi na Abdalla zilisababisha kugeukia mlengo mwingine, kwa mfano mwandishi amemchora Omondi kusajili chama cha upinzani.

**OBAMA Sr:** *Ker Omondi amesajili chama cha upinzani (uk.35).*

#### **4.5.3 Itikadi ya Ujamaa**

Ujamaa ni mfumo wa mpito katika maisha ya binadamu kuelekea Ukomunisti. Mfumo huu unatilia mkazo masuala ya kuupea unyonyaji, kuthaminiana, kuishi kindugu, kupa ubaguzi na kutojilimbikizia mali (Marx, 1959). Marx (1847) anabainisha vipindi mbalimbali vya maendeleo ya jamii tangu mwanadamu wa kwanza alipoumbwa mpaka sasa. Anavitaja vipindi hivyo kuwa ni ujima, utumwa, ukabaila, ubepari na ujamaa. Kipindi cha ujima ndicho kipindi cha kwanza cha maisha ya mwanadamu ambacho hakikuwa na tabaka la walionacho na wasionacho.

Watu wote walikuwa sawa kutokana na kumiliki kwa pamoja rasilimali zao. Vipindi vilivyofuata vya utumwa, ukabaila na ubepari vilitawaliwa na matabaka ya walionacho na wasionacho (Negri, 1982). Kipindi cha mwisho ni cha ujamaa ambacho hakina matabaka kutokana na rasilimali za umma kumilikiwa na jamii nzima. Hatua hii ya maendeleo ilifikiwa na jamii chache tu duniani kutokana na upinzani mkubwa kutoka kwa mataifa ya Kibepari kama Marekani, Uingereza, Ufaransa na washirika wao (Kennedy, 1978). Historia ya Ujamaa katika nchi ya Tanzania ilianza mwaka 1967 pale serikali ya chama cha Tanganyika Afrikan National Union (TANU) ilipoamua kutangaza rasmi kufuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kama itikadi ya kuongoza maamuzi ya kiuchumi na kisiasa (Chuachua, 2011). Ujamaa ni ile hali ya watu kufanya kazi pamoja na kugawana pato la nguvu yao kwa usawa. Naye Cleaver (1976) anaeleza kuwa, Ujamaa ni mfumo wa kiuchumi, kijamii au kisiasa unaowezesha umma kumiliki njia kuu za kuzalisha mali na mgawanyo wa haki wa mapato ulioasisiwa na Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius. K. Nyerere ili kuleta misingi ya usawa na haki miongoni mwa wanajamii. Ujamaa ni mfumo wa uchumi ambao ni hatua ya juu kuliko mifumo mingine yote ya uchumi. Mfumo wa ujamaa umeibuka baada ya tabaka lile lililokuwa linanyonywa na kugandamizwa kuamua kubadilisha hali yake duni na kufanya mipango maalum kupambana na tabaka lililokuwa linanyonya. Mapambano hayo yalibadilisha kanuni za umilikaji wa njia kuu zote muhimu za uchumi na madaraka ya kisiasa na serikali toka kwa tabaka la wachache na kuweka umilikaji wa madaraka hayo chini ya umma. Misingi ya uchumi wa kijamaa ambayo lazima izingatiwe na taifa linalojenga ujamaa ni hii ifuatayo: kumiliki kwa pamoja njia kuu muhimu za uzalishaji na ugawaji mali kiuchumi, kiushirika na kitaifa,

kuwoko demokrasia kamili, kuzingatia ugawaji wa mapato kijamaa, malipo kutokana na kiasi cha kazi mtu aliyofanya, kuwa na mipango ya uchumi ya maendeleo kwa taifa zima na kuwoko kwa mapinduzi halisi ya sayansi na ufundi. Tanzania ilichukua hatua sita katika kujenga uchumi wa kijamaa nazo ni: utaifishaji wa njia kuu muhimu za uchumi na uundaji wa mashirika ya umma, Ujamaa vijijini, madaraka kwa wananchi, Elimu ya kujitegemea na uwanzishaji wa viwanda mama (TUMI, 1990).

Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, imemtumia Omondi kama kiongozi anayependelea nchi ya Kenya kufuata itikadi ya kijamaa badala ya ubepari ambao unaonekana kuwanyonya damu wananchi.

OMONDI: *Ndugu Rais Nguruma, muarobaini wa maendeleo yetu ni kujenga uchumi wa kijamaa. Ubepari ni subiani atakaye wanyonya damu wananchi (uk.17).*

Omondi aliongea hayo baada ya kukataliwa na Rais Nguruma kujadili tena suala la Sessional Paper 10: Harambee na kanuni za Ujamaa wa Kiafrika. Abdalla aliungana na Omondi alipomweleza Rais Nguruma:

ABDALLA: *Mtukufu Rais, tatizo katika document hiyo ni sayansi. Neno Ujamaa na Harambee yamewekwa tu katika document hiyo ili kutekenya hisia na kufurahisha masikio ya watu. Lakini kwa kweli sera hiyo haihusu kujenga (uk.17).*

#### **4.5.4 Itikadi ya Ubepari**

Chiume (1980) ameelezea kuhusu falsafa ya ubepari wa kizungu katika makoloni kwamba ni watu wanaotawaliwa wafanye kazi chini ya serikali yoyote ya kigeni wakitosheka bila kulalamika. Ni watu wanaodhaniwa “kutokuwa na uwezo” wa kuendeleza rasilimali ya nchi yao wenyewe wakifundishwa kumenyeka na kupenda bidhaa zilizotengenezwa Ulaya ili wawe wanunuzi “wazuri”. Kwa msisitizo ubepari

ni maendeleo kwa utakaso kutoka ubwenyewe kama vile ubwenyewe ni maendeleo kwa utakaso kutoka utumwa ama ubepari si kitu kingine bali utaratibu wa kiutumwa wa waungwana.

Ubepari ni mfumo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii wa umiliki binafsi wa mali, biashara na viwanda kwa lengo la kutengeneza faida kubwa iwezekanavyo kwa kampuni na watu wenye kufanikiwa (Kennedy, 1978). Uchumi ni mali inayopatikana kutokana na amali za nchi au watu, au mfumo wa watu wa mapato na matumizi yao katika nchi. Raslimali mbalimbali katika taifa ndio uti wa mgongo katika kuleta maendeleo ya nchi. Katika uchunguzi wa tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, mtafiti alibaini kuwa, mtunzi anawasilisha itikadi ya kibepari. Kwa mfano, Rais Nguruma na Mboya wanakubaliana kujenga mfumo wa kibepari wa Kiafrika ama ujamaa wa kibepari, hili limethibitishwa na Mboya mwenyewe kwa kusema:

**MBOYA:** *Hatukupigania uhuru ili tugeuke Wamanyema ama wachawi wakulana sisi wenyewe kwa wenyewe. Mimi na Rais, Mzee Nguruma tunakubalia Kuhusu hili: kuhusu kujenga mfumo wa ubepari wa Kiafrika ama Ujamaa wa kibepari. Kwa lugha rahisi: mixed economy. Yaani mfumo Unaozingatia mahitaji ya wananchi: shule, maji, hospitali, kilimo, biashara, ujenzi WA nyumba bora, mishahara mizuri, amani, demokrasia ya kweli, haki za binadamu, maendeleo ya watoto Na akina mama; Utamaduni Na michezo, na kutokomeza uhasama na ukabila miongoni mwetu. Na huo siyo umanyema! Hayo ni maendeleo (uk.17).*

Dondoo hii inathibitisha kuwa, nchi inayotawaliwa na mabeberu humilikiwa na kunyonywa katika nyanja ya kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Msingi wa ubepari

ni kuwatumikisha watu kazi ya uzalishaji mali kwa ujira mdogo sana, unahakikisha faida kubwa inapatikana kwa ajili ya maendeleo yao, huduma za kijamii huwa kwaajili ya mabepari kwa mfano, barabara, maji na nishati ambazo zinaweza kutumika kwenye viwanda, usafirishaji na biashara. Mfumo huu usimamiwa na watu wachache lakini wenye nguvu kiuchumi.

#### **4.5.5 Itikadi ya Kikomunisti**

Ukomunisti ni mfumo wa kiuchumi, kijamii na kisiasa ambapo njia za uzalishaji mali zinamilikiwa na umma na mapato kugawiwa kufuatana na mchango wa nguvu na mahitaji ya kila mwananchi ama ni itikadi ya chama cha siasa kinachofuata mfumo huu.

(TUKI, 2004).Katika uchunguzi wa tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, mtafiti alibaini kuwa, mtunzi anawasilisha itikadi ya kikomunisti.

Nyerere (1974) anaeleza kwamba, nchi za Afrika zinaposhindwa kutoa msaada, huwa ni nchi za kikomunisti zinazojitokeza kusaidia. Sisi ni wakomunisti; sisi ni wazalendo tunatafuta uhuru. Tunatambua uko uwezekano kwamba hao wanaotusaidia wanaweza wakawa na shabaha zao tofauti. Kwa hiyo wapigania uhuru wanatumia silaha za kikomunisti, na wanapata mafunzo katika nchi za kikomunisti, na halafu kaburu na mreno wanatangaza kwa marafiki zao kwamba wanao ushahidi wa mapambano yao na wakomunisti. Hata watu wanaopenda usawa katika nchi hizo za magharibi wataacha kuwahurumia wapigania uhuru, kwa kusadiki kwamba wananchi hao wamo mifukoni mwa wakomunisti. Na polepole

mapambano hayo yatageuka kuwa mapambano yenye msingi wa imani kisiasa. Warusi na wakomunisti wa ulaya mashariki ndio watakaokuwa wazungu wanaosaidia Waafrika, na kwa kufanya hivyo watapunguza hatari ya mapambano haya kuwa mapambano ya rangi.

Kwa mfano, Ker Omondi (mwanasiasa maarufu) na Abdulla (mwanaharakati) walikuwa wanahubiri sana itikadi ya ukomunisti. Mtazamo huu ulitofautiana na wanasiasa wengine nchini Kenya. Mwandishi anabainisha hili kwa kumtumia mwanahabari wa KBC na Televisheni pale alipomuuliza swali Mheshimiwa Tom Mboya kwamba anaamini nini, ukomunisti au ubepari?

MWANAHABARI: Mheshimiwa, *wewe unaamini nini? Ukomunisti au ubepari?*

MBOYA: *Mmi naamini Mungu!.....Najua mzee wetu Omondi na viongozi wengine Mashuhuri kama Abdulla wanahubiri sana ukomunisti. Lakini mimi Mboya nasema: Wakenya tuko tayari kufanya biashara na Warusi na hata Wachina. Jambo kubwa sio ism. Jambo kubwa ni maendeleo kwa watu wote. Kupigana na maadui watatu: Ujinga, Umaskini na Maradhi (uk.12).*

Kanoga ni miongoni wa wanasiasa wanaopinga sera ya ukomunisti. Mwandishi amemtumia Kanoga na wenzake kuibeza itikadi inayofuatwa na akina Abdulla na Omondi kiasi cha kufananishwa na nchi ya Tanzania iliyokuwa inafuata siasa ya Ujamaa na kujitegemea. Kwa kudhihirisha hili, Kanoga anasema:

KANOGA: *Akitaka kujenga Ukomunisti si aende Tanzania kwa Nyerere wanakovaaviatu vya matairi ya gari! (uk. 15).*

Mwandishi Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amemtumia Omondi kama mwanasiasa anayesimamia upande wa itikadi ya ukomunisti na kupinga itikadi zingine kama vile ubepari. Mtafiti alibaini kuwepo itikadi hii kupitia mkutano wa Rais Nguruma na mawaziri. Omondi anamweleza Rais Nguruma kwamba, maendeleo ya nchi yatajenga uchumi wa kijamaa.

OMONDI: *Ndugu Rais Nguruma, muarobaini wa maendeleo yetu ni kujenga uchumi wa kijamaa. Ubepari ni subiani atakaye wanyonya damu wananchi (uk.18).*

Mwandishi amemchora Rais Nguruma jinsi alivyo jawa na hasira baada ya kusikia maneno ya Omondi kuhusu anavyohusudu itikadi ya ukomunisti na kutounga itikadi nyingine kama ubepari. Rais alianza kusema kwa hasira kali:

NGURUMA: *Ninyi watu! Mnataka ngoma za masikio yangu zipasuke kwa mirindimo ya ngoma za ukomunisti? Mnataka mboni ya macho yangu ziingie upofu kwa moshi wa itikadi za ukomunisti? Mnataka damumwilini mwangu isite kutiririka kwa sababu ya sumu ya moma wa kikomunisti? Mnataka akili zangu ziote magugu ya wazimu kwa sababu ya nyimbo za mahepe ya ikomunisti? Ama mnataka radi na rada za ukomunisti zipasue moyo wangu na kuongeza kasi ya shinikizo la damu ndani ya kigoda hiki cha ufalme? Shetani wa magharibi tunamjua; shetani wa kikomunisti hakuna Mkenya anayemjua ila Mheshimiwa Omondi na Abdulla! (uk.18)*

Kutokana na maelezo hayo hapo juu ni dhahiri ukomunisti hulenga kuifikisha jamii katika hali isiokuwa na matabaka ya matajiri na maskini yaani watu wenye mali nyingi kuliko wengine. Vyama vya Wakomunisti vilifaulu kushika serikali katika Urusi tangu 1917, katika Umoja wa Kisovyeti tangu mnamo 1920/1924 halafu katika nchi za Ulaya ya Mashariki tangu 1945/46. Katika China, Korea ya Kaskazini na Vietnam ya Kaskazini Wakomunisti walitawala tangu mnamo

1948/49. Vyama mbalimbali katika nchi kadhaa za Afrika vilifuata mfumo wa Wakomunisti kwa namna fulani na kushika utawala kwa miaka kadhaa.

#### **4.5.6 Itikadi ya Dini**

Jamii za Kiafrika zimekuwa zikiamini katika dini kwa kipindi kirefu hata kabla ya ujio wa Wakoloni. Waafrika walikuwa wakiamini katika dini za asili na kufanya ibada katika mapango na chini ya miti mikubwa huku wakiamini katika miungu na si katika Mungu mmoja kama ilivyo katika dini za Kikristo na Kiislamu (Mbiti, 1956). Utafiti ulibaini kuwa dini ni Imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumba ambaye aliumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kilichomo.

Pia ni mfumo fulani wa dini hii na njia ya kuabudu, kusali, na kuhemshimu huyo muumba. Mwandishi katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amemtumia Musili kuwa ni Mungu pekee mwenye uwezo wa kukifinyanga kiumbe na kukitia uhai kikiwa tumboni mwa mama yake. Kwa kuthibitisha hili, mtafiti alibainisha maongezi ya Ndiege na rafiki yake Musili walipokuwa wanakunywa pombe.

**MUSILI:** *Hofu ya wanagenzi wa kuitwa mzazi. Lakini ni hofu na mashaka yasiyokuwa na msingi. Tendo lililochochea mapenzi lilikuwa takatifu. Naye Rabuka alipolitakabali, alinyoosha mkono toka mbinguni, Akafinyanga kiumbe na kutia uhai ndani ya wako malkia (uk.5).*

Hata baada ya Awour, kujifungua mtoto, alimpa jina la Odhiambo. Lakini Ndiege, baba mtoto alitaka ampeleke kanisani ili abatizwe kwa jina la kikristo. Ndiege ana mweleza Musili:



NDIEGE: *Tutakapompeleka kanisani, kule Romani Katoliki, mimi Nitamwambia padiri ambatize, aitwe: Thomas (uk.8).*

Mwandishi wa tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016), amemtumia Wanjiru mke wa Kanoga kama mwanamke mlokole, anamtaka mumewe kanoga kumgeukia yesu kristo. Wanjiru anasema:

WANJIRU: *Na kila siku nikikuambia mume wangu mgeukie Yesu, uwe mlokole, Yesu awe mwokozi wako. Lakini unakataa! Sasa leo umeiona faida ya ulokole! Kesho lazima nikupeke kwa pasta wetu akuombe. Hii nyumba lazima ipate buruji la agano la chumvi (uk.46).*

Wanjiru alimsimulia Wairimu mkasa wote alioupata Kanoga, naye Wairimu akawasimulia Mboya na Obama Sr aliyokumbananayo Kanoga.

WAIRIMU: *Alinambia ana mpango wa kumpeleka Kanoga kanisani akaombewe!(uk.50).*

Katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amemtumia Pamela mke wa Tom Mboya, kuwa ni mama mvumilivu na anayemtegemea Mungu katika maisha yake na familia yake. Mtafiti alilibaini hili baada ya kuulizwa swali na mwandishi wa habari Sofia:

PAMELA... *Lakini kwa vyovyote vile, nadhani jambo kubwa ni Kumwomba na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Wimbo wetu wa Taifa Unasisitiza suala la kumtegemea Mungu (uk.66).*

Pamela na watu waliomzunguka walianza kuimba wimbo wa Taifa la Kenya.

*Ee, Mungu nguvu yetu  
Ilete Baraka kwetu  
Haki iwe ngao na mlinzi  
Na tukae na undugu, amani na uhuru  
Raha tupate na ustawi (uk.66-67)*

Kwa ujumla dini kwa kipindi kirefu cha maisha ya mwanadamu imekuwa kitovu cha ustaarabu wa jamii mbalimbali. hivyo kadiri jamii inavyobadilika ndivyo mambo mengi huongezwa au kutolewa katika mapokeo yake ili hali kuakisi mazingira ya nyakati. Katika kipindi cha sasa, kumekuwepo kwa jitihada mbalimbali zinazopokea na kuchunguza misingi ya dini na maisha. Mwandishi amemchora Ndiege kama muumini wa Roman Katoliki hakuridhika na jina la Odhiambo alilopewa mwanaye alisema kwamba, watakapompeleka kanisani, kule Romani Katoliki, atamwambia Padri ambatize mwanaye kwa jina la Thomas.

#### **4.5.7 Itikadi ya Utamaduni**

Utamaduni ni mila, asili, jadi, na desturi za kundi la jamii fulani. Itikadi hii inaweza kujitokeza katika sura mbalimbali, kwa mfano, katika sherehe kama vile harusi, misiba, mila na desturi, lugha na hata matambiko (Mbiti, 1956). Suala la itikadi ya utamaduni katika tamthiliya ya Mbogo (2016) Nyota ya Tom Mboya linajibainisha kupitia uwepo wa ngoma mbalimbali katika tamthiliya hiyo. Katika uchunguzi wa tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya, utafiti huu umebaini kuwa, tamthiliya hiyo inaibua itikadi ya kiutamaduni katika jamii. Kwa mfano, mwandishi ametumia ngoma katika sherehe ya kuzaliwa mtoto, ngoma na vigelegele zinasikika; watu wanacheza; wakimshukuru Mungu kuwa: mtoto amezaliwa (uk.8). Katika mila na desturi za Kiafrika, sherehe kama hizi ni sehemu ya utamaduni wa Waafrika ambayo huonyesha furaha na hisia ya kupata mtoto.

Kazi ni sehemu inayoweza kuwakutanisha watu wenye itikadi tofautitofauti na waliotoka maeneo mbalimbali. Kwa mfano, mwandishi amemchora Musili pamoja na kukutana na watu wenye lugha na tamaduni tofautitofauti katika kazi ya kukata mkonge bado walijisikia kitu kimoja. Musili anaongea na Ndiege:

MUSILI: *Lakini unajuwa: hii kazi ya kukata mkonge, pamoja na taabu zake; Imekuwa fursa ya kuyakutanisha makabila toka kote nchini Kenya(uk.6).*

NDIEGE: *Ni kweli. Watu wenye lugha na tamaduni tofauti tofauti, baada yamuda wanajisikia kama kitu kimoja (uk.6).*

MUSILI: *Kama taifa moja (uk.6).*

Imekuwa ni utamaduni kwa Waafrika kutumia wasanii wa ngoma za asili kumpokea na kumkaribisha mgeni ama kiongozi yeyote wa kitaifa ili aweze kujisikia yupo nyumbani, hii ni pamoja na kupata ladha tofauti na ile ambayo ameizoea. Mwandishi Mbogo katika tamthiliya yake ya Nyota ya Tom Mboya, ametumia vikundi vya ngoma kama burudani kwa wageni na watu waliofika kumpokea mgeni. Mtafiti alilibaini hili pale Wairimu alipokuwa mshereheshaji:

WAIRIMU: *MheshimiwaTomMboya, Mheshimiwa Balozi wa Marekani nchini Kenya. Mheshimiwa Baraka Obama. Mabibi na Mabwana. Itifaki imezingatiwa. Ratiba ya sherehe zetu inaanzana burudani; nami bila kupoteza wakati, namkaribisha Msanii maarufu hapa nchini, bwana KI-PRO-TI-CHI! Piga kelele na shangwe kwa Hurarambee Afrika Drums!(uk.51).*

Kitendo cha kuwepo kwa vikundi vya ngoma na burudani katika mapokezi ya balozi wa Marekani ni utamaduni wa waafrika kumkaribisha mgeni kwa shangwe, vigeregere na bashasha ili aweze kujisikia yupo nyumbani na awe na amani.

Mshereheshaji Wairimu alimkaribisha msanii maarufu nchini Kenya KI-PRO-TI-CHI kuuburudisha umati wa watu waliofika uwanja wa ndege kumlaki balozi wa Marekani.

#### 4.5.8 Itikadi Katika Mapenzi

Itikadi ya mapenzi inajitokeza pia katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, mtafiti amebaini kuwepo kwa itikadi ya mapenzi, kwa mfano mwandishi wa tamthiliya hii amemtumia Pamela kama mama mwenye mapenzi mema tena ya dhati kwa mume wake Tom, kwa kutaka aachane na siasa ili abaki na yeye hii ni kutokana na Tom Mboya muda mwingi kuwa mbali na familia. Mwandishi anabainisha kwa kusema:

PAMELA: *Nasema: Natamani ningekuwa na uwezo; ningekuwa na ujasiri wa kumwamuru Tom ampe talaka huyu mwanamke anayeitwa siasa. Lakini siasa! Kila kukicha siasa. Ukilala siasa. Wakati Pamela anaongea machozi yalikuwa analia (uk.34).*

Hapa inaonyeshwa kuwa, Tom Mboya kwa mapenzi makubwa aliyonayo kwa mke wake Pamela, anakaa na anamkumbatia huku akimbembeleza. Tom Mboya anasema.

MBOYA: *Basi tulia... pole....(uk.34).*

Aidha Tom Mboya baada ya kupigwa risasi, Pamela alipiga yowe, akamshika Mboya kabla hajaanguka... akayumbanaye... akawa amezidiwa... wakaanguka chini... wote wawili... kisha anakata roho (uk.69). Kwa hili mwandishi anadhihirisha kuwepo kwa mapenzi ya dhati kwa mume wake Tom Mboya.

#### 4.5.9 Itikadi ya Ubaguzi wa Kijinsia

Malezi na uzazi ni masuala muhimu katika makuzi ya watoto na hatimaye vijana wa taifa la kesho (Alhabib, 2012). Watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakipaza sauti zao kote duniani kupinga ubaguzi wa kijinsia. Jamii nyingi hususani za Kiafrika zimekuwa na ukiukaji mkubwa kwa kuwabagua watoto kijinsia. Wazazi wamekuwa wakiwajali sana watoto wa kiume na kuwaacha wale wakike kwa misingi ya kiutamaduni, dini au itikadi. Mwandishi Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, amemtumia Ndiege kuthibitisha kauli hii pale aliposema:

NDIEGE: *Ni kweli. Na sijui ama nitapata simba anaye unguruma? Ama tausi Ambaye kazi yake itakuwa kutingisha manyoya ya kiuno chake akisubiri Kunyakuliwa na mabeberu barubaru wa kijaluo (uk.6).*

Ndondoo hii inaonyesha kumuinua na kumjali mwanaume na kumfanya mwanamke kama chombo cha starehe ambapo kiuhalisia ni kumnyima haki mtoto wa kike.

Naye Musili rafiki yake Ndiege, alimjibu Ndiege kwa kusema: *Ama wawindaji shujaa wa Kikamba. Kauli ya Musili haikumpendezesha Ndiege. Mwandishi amemchora Ndiege alivyokasirika kwa kusema:*

NDIEGE: *We! Musili usinichafuwe. Usinilizie ndege mbaya (uk.7).*

MUSILI: *Kuhamanika kwako ni kani iwezayo kuchochea hasira ya wahenga. Mtoto ni mtoto, awe msichana ama mvulana. Fauka ya hao, hao wanaojaza nimama zetu; sio sisi (uk.7).*

Mtafiti aliendelea kubaini kuwepo kwa itikadi ya uzazi katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016), kwa mfano, mwandishi amemtumia Ndiege alivyokwa anahaha ni mtoto wa jinsi gani atakayezaliwa. Furaha ya Ndiege ilijidhihirisha baada ya kusikia Awouri amejifungua mtoto wa kiume. Mwandishi anasema:

NDIEGE: *Tayari nimepata mtoto.*

MUSILI: *Bila shaka amezaliwa Msumbi! Amezaliwa simba .Baada ya kukabidhiwa mtoto, Mwandishi anaonyesha furaha aliyokuwa nayo Ndiege, anamkagua, anatabasamu. Anamwombea kwa Mungu kwa lugha ya Kijaluo (uk.8).*

Kwa maelezo haya inasadifu jamii nyingi hususani za Kiafrika bado zina imani potofu ya kusadiki kwamba mtoto wa kiume ndio mtoto na mtoto wa kike ni wa kuolewa tu hivyo msaada wake ni mdogo katika familia. Itikadi ya namna hii haifai kuigwa na jamii, jamii inatakiwa kupatiwa elimu ya uzazi na ustawi kwa ujumla. Wito unatolewa kwa watu wote kujali na kuwajibika kwa watoto wao wa kiume na wakike bila ubaguzi, hii itajenga jamii katika kuheshimiana na kulinda hazi za watu wote na kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake.

#### **4.6 Uhusiano Kati ya Siasa na Itikadi Katika Tamthiliya ya Nyota ya Tom Mboya**

Uhusiano ni hali ya kuwa na fungamano. Fungamano katika umoja baina ya watu, ushirikiano na uambatano unaweza kuwa mzuri au mbaya.

Lengo mahususi la tatu katika utafiti huu ni kubaini uhusiano uliyopo kati ya siasa na itikadi, mtafiti ameshughulikia uwepo wa uhusiano uliopo kati ya siasa na itikadi. Kutokana na matini mbalimbali yaliyopitiwa na mtafiti, imebainika kuwepo kwa uhusiano wa siasa na itikadi. TUKI (2004) wanasema kwamba, itikadi ni imani au mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au uchumi lakini wanaendelea kufafanua kwamba, siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi la jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi,

utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo au mbinu ya utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa.

Katika kuchunguza uhusiano wa siasa na itikadi kupitia tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, utafiti huu umebaini kuwa mwandishi anaibua mambo mbalimbali yanayohusianisha siasa na itikadi kwa kuzingatia misingi ya siasa na itikadi kama vile; ujenzi wa uchumi, mfumo wa siasa na itikadi katika maisha ya binadamu na jamii kwa ujumla.

#### **4.6.1 Ujenzi wa Uchumi, Mfumo wa Siasa na Itikadi katika Jamii**

Uchumi ni jumla ya shughuli zote za binadamu zinazolenga kutosheleza mahitaji yao. Ni hasa uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa bidhaa pamoja na kutolewa kwa huduma kwa njia mbalimbali. Ni mali iliyopatikana kutokana na amali za nchi au watu. Mwandishi wa *Nyota ya Tom Mboya* amebainisha wananchi wa Kenya walivyojishughulisha na uzalishaji mali, hii imejidhirisha Musili na rafiki yake Ndiege.

MUSILI: *Lakini unajua: hii kazi ya kukata mkonge, pamoja na taabu zake; imekuwa fursa ya kuyakutanisha makabila toka nchini Kenya (uk.6)*

NDIEGE: *Ni kweli. Watu wenye lugha na tamaduni tofauti tofauti, baada ya muda wanajisikia kama kitu kimoja (uk.6).*

MUSILI: *Kama taifa moja (uk.6).*

Maelezo haya yanathibitisha kwamba ili jamii iweze kuinua uchumi wake na kwa taifa kwa ujumla sharti ifanye kazi kwa juhudi, maarifa na bidii na kushirikiana kijamaa aidha kile kinachopatikana kigawiwe sawa.

Mwandishi amewaibua Abdalla na Omondi, kuitaka jamii kuujenga uchumi wa kijamaa ambao wanaamini hiyo ndiyo njia pekee ya kupata maendeleo na kuachana na dhana ya kuongea kinadharia tu bali vitendo yaonekane, hili lilijitokeza kwenye kikao cha mawaziri ambapo Abdulla na Omondi walipokuwa wanaitetea sera ya ujamaa na kupinga ubepari. Kwa maneno yake Abdalla anasema:

*ABDALLA: Mtukufu Rais, tatizo katika document hiyo ni sayansi. Nenoujamaana Harambee yamewekwa tu katika document hiyo ili kutekenya hisiana kufurahisha masikio ya watu. Lakini kwa kweli sera hiyo haihusu kujenga uchumi wa kijamaa (uk.17).*

Kwa maelezo haya mtafiti anaona kuwa nchi au kundi la jamii fulani inaweza kuwa na chama chake cha siasa ambacho kinatawala kwa kufuata itikadi fulani ambao ni msingi kuendesha nchi kiuchumi, kiutamaduni na kifikra. Kwa mfano, nchi ya Tanganyika kwa sasa Tanzania chini ya Rais Julius K. Nyerere aliongoza kupitia chama cha TANU kwa itikadi ya siasa ya Ujamaa na kujitegemea.

Katika tamthiliya ya Nyota ya *Tom Mboya*, mwandishi amewachora wanasiasa na wanaharakati nchini Kenya jinsi walivyosimamia itikadi zao. Kuthibitisha maelezo haya mwandishi anasema:

**MWANAHABARI1:** *Mheshimiwa, wewe unaamini nini? Ukoinisti au Ubepari?*

**MBOYA:** *Mimi naamini Mungu!*

**MBOYA** ....*Najua mzee wetu Omondi na viongozi wengine mashuhuri kama Abdulla wanahubiri sana ukoinisti (uk.12) Mboya anaendelea kuongea, Mimi na Rais Nguruma tunakubaliana kuhusu kujenga mfumo wa Kibepari wa Kiafrika ama ujamaa wa kibepari. Kwa lugha rahisi: mixed economy. Yaani mfumo unaozingatia mahitaji ya wananchi (uk.13).*



Huu ni uthibitisho kuwa viongozi wanaweza kuwa katika chama kimoja cha siasa lakini wakawa na mtazamo tofauti kwa kuamini ni itikadi ipi itakayo mfikisha katika malengo yake. Kutofautiana kwa itikadi miongoni mwa wanasisa umesababisha mivutano, mikwaruzano, minyukano na hata nchi kuingia kwenye vita vya kikabila au kidini. Mwandishi wa tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* (2016) anasema:

TUTA: *Tazama jana pale kwenye mkutano. Bila woga, tena ana kwa ana, Abdulla alimshambulia Rais, akikemea, akikebehi na kubeza mfumo tunaotaka kuujenga (uk.15).*

KANOGA: *Akitaka kujenga ukomunisti si aende Tanzania kwa Nyerere Wanakovaa Viatum vya matairi ya magari!(uk.15)*

OMONDI: *Ndugu Rais Nguruma, muarubaini wa maendeleo yetu ni kujenga uchumi wa kijamaa. Ubepari ni subiani atakayewanyonya damu wananchi. Ubepari ni koleo itakayowazika wakulima na wafanyakazi kaburini (uk.17).*

Maelezo haya yanabainisha Rais Nguruma alivyotofautiana kiitikadi na akina Abdulla na Omondi lakini wakiwa kwenye utawala mmoja. Viongozi hawa walikuwa na marafiki kutoka mataifa ya nje, mataifa haya yaliweza kutoa misaada mbalimbali katika vyama rafiki vinavyofuata itikadi kama ya kwao. Kwa mfano, Tom Mboya alikuwa kipenzi cha Marekani (CIA), Abdulla na mzee Omondi marafiki wao walikuwa Warusi na Wachina (KBG) ambapo Wamarekani waliamini mfumo wa kibepari ndio utakaofaa kuujenga uchumi ambapo waliongozwa na itikadi zao. Hili linathibitishwa na Kanoga, Wanjiru, Tuta na Chatu kwa kusema:

KANOGA: *Abdalla alikuwa kuwadi muhimu wa kueneza itikadi za Kimarx. Aliwafanyia Warusi kazi nzuri kule Msumbiji (uk.40).*

WANJIRU: *Lakini si mnajua pia kuwa Tom Mboya ni kipenzi cha CIA (uk.41).*

TATU: *Sawa kabisa. Na baya zaidi ni kuwa: CIA inafanya juhudi za ziada Kung'oa Mzee Nguruma ili Tom awe Rais (uk.41)*

wakati CIA inapambana kung'oa Mzee Nguruma ili kumsimika Tom kuwa Rais, Warusi na Wachina hawakumtaka Tom Mboya kwa sababu ya siasa zake za CIA. Chatu amethibitisha hili kwa kusema:

CHATU: *Nasikia Wachina na Warusi hawamtaki Mboya kwa sababu ya siasa zake za CIA (uk.62).*

Urusi na Wachina waliamini ukoministi, hali hii ilisababisha kuwepo kwa vita baridi miongoni mwa mataifa haya makubwa duniani. Mwandishi amemtumia Kanoga kubainisha ushirika waliokuwa nao Ker Omondi, Abdulla na KBG pale Wanjiru na Kanoga wanaposema:

WANJIRU: *Na hili ndilo lililochochea hasira za CIA. Na wakati Abdullaakirukaangani, Setlite za Marekani zimekuwa zinanasa nakuhifadhi ujasusi wake wote (uk.40).*

KANOGA: *Ker Omondi kisha sajili chama cha upinzani. Na KBG na Bejini bado wamevaa majoho meusi wakiomboleza. Abdulla alikuwa kuwadi muhimu wa kueneza itikadi za Kimarx. Aliwafanyia Warusi kazi nzuri kule Msumbiji (uk.40).*

Ushirika wa nchi hizi haukuishia kwenye kutoa misaada nchini Kenya, bali nchi za kikomonisti zilitanua wigo wa kuzikomboa nchi zilizokuwa kusini mwa bara la Afrika. Mwandishi wa tamthiliya ya Tom Mboya anasema:

CHEGA: *Ndiyo maana safari zake za Tanzania, Msumbiji na Angola Zilikuwa haziishi (uk.40).*

Maneno haya yanaakisi hotuba ya Mheshimiwa, Rais Dkt. John.P.J.Magufuli aliyoitoa Julai, 16 2018 Kibaha Pwani alipokuwa anaweka jiwe la msingi wa ujenzi wa chuo cha uongozi na itikadi. Magufuli alisema kwamba, chuo hiki kinajengwa chini ya vyama sita vilivyoshiriki katika ukombozi wa bara la Afrika yaani CCM (Tanzania), ANC (Afrika Kusini), SWAPO (Namibia), MPLA (Angola), Msumbiji (FRELIMO) na ZANU-PF (Zimbabwe) kwa kushirikiana na chama cha kikoministi cha Kichina ambacho kimekuwa rafiki wa siku nyingi, kwani kimekuwa kikitoa misaada mingi ikiwemo silaha, vifaa vya kijeshi, mafunzo ya itikadi na propaganda katika vyama rafiki. Rais Magufuli aliendelea kusema, suala la uongozi na itikadi ni miongoni mwa matatizo makubwa katika zama hizi za demokrasia ya vyama vingi, kwani vyama vingi vya kisiasa vinavyoanzishwa vinakosa viongozi wenye uzoefu na itikadi inayoeleweka.

Kwa maelezo haya ni dhahiri chama chochote cha kisiasa ni sharti iwe na itikadi yake kama dira na mwelekeo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kama vile; uchumi, utamaduni, imani na kufanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya wananchima kwa ujumla.

Siasa ni sanaa au ayansi ya kutawala na kuongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serkali. Katika kuongoza na kutawala, serikali hudhibiti masuala yake ya ndani na yale ya nje ili kuleta uwiano sahihi utakaofanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya wananchi. Hivyo basi, tunaposema: kutawala na kuongoza

tunamaana kwamba, siasa ndio huamua hatima ya Nyanja nyingine za maisha. Siasa ya nchi ndio inaamua ni aina gani ya uchumi iwepo nchini, mfumo na mpango mzima wa masuala ya kijamii uweje nakadhalika. Hivyo ni sawa na kusema kwamba, sirahisi kutenganisha siasa na mfumo mzima wa maisha ya jamii. Itikadi ni dhana ambayo imeelezwa na wataalamu mbalimbali kutokana na ukweli kuwa kila jamii inaongozwa na itikadi fulani katika kufanikisha maisha yake ya kila siku.

#### **4.7 Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti aliwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti. Katika lengo mahususi la kwanza lililohusu Siasa mtafiti amebainisha kuwepo kwa siasa na harakati za ujenzi wa jamii mpya, uongozi bora na imani kwa wananchi, ukombozi wa nchi za Afrika, elimu na maendeleo, siasa za ukabila, hofu na tama ya madaraka, kujitoa muhanga, nafasi ya mwanamke katika siasa, Uhusiano wa nchi za Afrika na zile za magharibi na Vibaraka wa kisiasa na umwagaji damu. Lengo mahususi la pili lilihusu itikadi, ambapo mtafiti amebainisha kuwepo kwa itikadi za, kishirikina, mapinduzi, ujamaa, ubepari, kikomunisti, dini, utamaduni, mapenzi na ubaguzi wa kijinsia. Aidha katika lengo mahususi la tatu mtafiti kafafanua uhusiano uliyopo kati ya siasa na itikadi, data alizozichambua katika matini zilimwezesha kubaini uwepo wa uhusiano huo.

## SURA YA TANO

### 5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

#### 5.1 Utangulizi

Emmanuel Mbogo ni mwandishi mashuhuri wa tamthiliya, riwaya na hadithi fupi. Kazi hizi ni bora zilizojaa mafunzo, maadili, nasaha na uzalendo kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla. Mtafiti alitumia tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kuchunguza masuala ya Siasa na Itikadi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, masuala ya kisiasa yanayo sawiriwa katika tamthiliya hii yametoa mchango mkubwa kiuchumi, kisiasa, kiitikadi na kiutamaduni nchini Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla. Haya yamebainika kupitia malengo mahususi matatu yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu. Muhtasari wa kila lengo mahususi ni huu ufuatao.

#### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Tasinifu hii imefanywa kwa nia ya kutimiza malengo matatu ambayo yalikuwa ni kubainisha siasa zilizojitokeza katika tamthiliya ya Mboya (2016) *Nyota ya Tom Mboya*, kubainisha itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya Mboya (2016) *Nyota ya Tom Mboya* na kufafanua uhusiano uliyoko kati ya siasa na itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya Mboya (2016) *Nyota ya Tom Mboya*.

##### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Tasinifu hii imewasilisha na kuchambua masuala ya siasa yaliyojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kwa mafanikio makubwa. Mtafiti amebaini

kuwepo kwa siasa na harakati za ujenzi wa kijamii. Katika tasinifu hii imebainika walikuwepo wanasiasa na wanaharakati wenye kuamini itikadi tofautitofauti mfano, Abdulla na Omondi waliamini katika itikadi ya ukoministi wakati Tom Mboya na wenzake waliamini ujamaa wa kibepari. Uongozi bora na imani walionao wananchi kwa viongozi wao, tasinifu imebaini kuwepo suala hili pale Rais Nguruma alipoanika hisia na imani kwa Tom Mboya, hii si kwa rais tu bali hata wananchi wa makabila tofauti walimkubali Tom Mboya hata kuthubutu kumwita mkombozi wao pia walikuwa wana mlaki kwa wingi pale uwanja wa ndege. Lakini suala la ukombozi wa nchi za bara la Afrika limebainishwa na tasinifu hii, viongozi wa bara la Afrika waliweza kukutana mara kadhaa kuzungumzia suala la kujikomboa kisiasa na kiuchumi, kwa mfano Rais Kwame Nkrumah wa Ghana alitisha kikao cha viongozi wa nchi za bara la Afrika huko Accra, pia mkutano mwingine ulifanyikia Addis Ababa-Ethiopia. Tasinifu hii imebainisha kuwepo kwa Elimu na maendeleo, mwanasiasa Tom Mboya aliwatafutia wanafunzi ufadhili wa kusoma marekani, alifanikiwa kupata nafasi (Scholarship) 1000 kwa mpango wa Students airlift kwa ajili ya maendeleo ya vijana na Taifa la Kenya. Vilevile siasa za ukabila umebainishwa katika tasinifu hii, kwa mfano, katika nchi ya Kenya imejitokeza kuwepo na siasa za ukabila, mwandishi wa tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* amewachora wanasiasa walivyokuwa wanapigana vijembe na hata kuchafuana kwa sababu ya ukabila. Mwanasiasa Ker Omondi alidiriki kuwaeleza wapiga kura kutomchagua Tom Mboya kwa sababu sio kabila lao, kwa hili halikubaliki ni ukiukaji wa haki za binadamu, kidemokrasia kila raia mwenye sifa anayo haki ya kuchagua kiongozi ampendae na kuchaguliwa kuwa kiongozi.

Hofu na tamaa ya madaraka imebaishwa katika tasnifu hii, wanasiasa Kanoga, Chega na Tuta walionekana kuwa na uchu wa madaraka, hali hii ilianza kujitokeza kwenye kikao cha mawaziri ambacho kiliitishwa na Mheshimiwa Rais Nguruma, Kanoga na wenzake waling'ang'ania kuingizwa ajenda ya kubadili katiba ya nchi, lengo kubadili baadhi ya vifungu ili waweze kumbana Tom Mboya asiweze kushika madaraka endapo Rais Nguruma atafariki, lakini akiwa kwenye mkutano wake wa kampeni, Ker Omondi alionyesha hofu ya jimbo kuchukuliwa na Tom Mboya pale alipo wataka wananchi wasimpigie kura ya ubunge Tom Mboya katika jimbo la Nairobi badala yake wampe Owino Okaka. Tasnifu imebainisha uwepo wa watu kujitoa muhanga katika harakati mbalimbali, kwa mfano Tom Mboya alijitoa muhanga kupigana na maadui watatu: Ujinga, umasikini na maradhi lengo ni kuwapatia maendeleo wananchi wake, adui mmoja alishaanza kupambana ambaye ni ujinga kwa kuwapeleka wanafunzi 1000 kusoma Marekani. Inaonesha jinsi watu wa Kenya walivyojitoa muhanga na kuwa tayari kupoteza uhai wao kwa ajili ya kuikwamua nchi mikononi mwa mkoloni. Nafasi ya mwanamke katika harakati za siasa nayo imebainishwa katika tasnifu hii, Pamela mke wa Tom Mboya alikuwa anabaki upweke wakati mumewe yupo kwenye majukumu yake ya kisiasa na kiserikali, alifikia hatua ya kuhofia uhai na usalama wa mumewe hata hivyo alimhakikishia bwanake atakuwanaye bega kwa bega katika shughuli zake za kisiasa na kumwahidi kuwa atakuwa nae wakati wa mvua, jua hadi mwisho wa dunia. Uhusiano wa nchi za Kiafrika na zile za Magharibi umejitokeza kwenye tamthiliya Mbogo(2016) *Nyota ya Tom Mboya*, wanasiasa walikuwa na washirika wao kutegemeana na utangamano wa itikadi yao, kwa mfano, wanasiasa waliofuata siasa za kibepari walishirikiana na taifa la Marekani na wale waliofuata siasa za

kikomunisti walifungamana na nchi za Urusi na China. Suala hili ni hatari sana linaweza kuliingiza taifa kwenye ukoloni mamboleo kwani wakoloni hawa wanatoa misaada kwa ajili ya kukipata kile wanachokitafuta (mali), mataifa haya ya kimagharibi hutumia kila hila ikiwemo kuweka vibaraka wao, na kwa hakika vibaraka hawa huweza kusababisha umwagikaji wa damu zisizo na hatia. Kwa mfano tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* imewachora Duma na Chatu walivyomuua Tom Mboya kwa kumpiga risasi baada ya kutumiwa na mataifa ya Urusi na China yaliyoko chini ya shirika lao la KGB, hii ilitokana na kulipa kisasi baada ya CIA kumuua mwanaharakati Abdulla.

### **5.2.2 Lengo Mahususi la Pili**

Lengo mahususi la pili lilikuwa ni kubainisha masuala ya itikadi zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Itikadi zilizojitokeza ni; Ushirikina, Ushirikina ni hali au tabia ya kuamini mambo ya uchawi, mizimu nk. Jamii nyingi za Kiafrika zinaamini sana mambo ya ushirikina hili linajitokeza sana hata kwa viongozi wa serikali na wanasiasa, walio wengi hufanya hivyo ili kupata madaraka katika kada zao. Kanoga alibwia bwimbwi la Iluminata alilopewa na Nabii kwa kuaminishwa kwamba hilo bwimbwi lilikuwa na nguvu ya ulumbi katika hotuba. Kwamba angeweza kuwa mshindi kwa kila uchaguzi hivyo hakuna mwanasiasa yeyote atakayefua dafu kwake. Mapinduzi ni mabadiliko ya haraka katika mfumo wa maisha ya jamii ambao huwanufaisha watu waliowengi. Tom Mboya alithubutu kufanya mapinduzi katika suala la elimu, alipambana hadi alipofanikiwa kupata nafasi 1000 ya wanafunzi kwenda masomoni Marekani. Ujamaa nao umebainishwa katika tasnifu hii, ujamaa ni mfumo wa kiuchumi unaowezesha mali na mgawanyo



wa mapato. Tanganyika kwa sasa Tanzania chini wa Rais JK Nyerere ilifuata siasa ya ujamaa na kujitegemea kwa misingi na imani ya binadamu wote ni sawa. Mwanaharakati Abdulla alipenda sera ya ujamaa itekelezwe kwa vitendo na sio ibakie kwenye makaratasi tu, Omondi kwa msisitizo anaamini muarubaini wa maendeleo ya Wakenya ni kujenga uchumi wa kijamaa na sio ubepari. Dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binadamu na Mwenyezi Mungu. Itkadi ya dini imebainishwa katika tasnifu hii. Ndiege anatambua uwepo wa Mungu, baada ya kuzaliwa mtoto anafurahi hususani kuona ni mtoto wa kiume, anamwomba kwa Mungu na kuahidi kumpeleka kanisani, kule Romani Katoliki, na angemwomba Padiri ambatize, aitwe: Tomas, lakini Wanjiru alikuwa mllokole mara kwa mara alipendelea kuimba nyimbo za dini aidha alimtaka mmewe Kanoga aokoke ili aweze kuondokana na masahibu ya dunia hii. Utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha wao na jamii nyingine (WEU, 1997). Jamii nyingi za Kiafrika hujibainisha kwa kushikilia tamaduni zao, kwa mfano, nchini Kenya watu hufahamiana kwa lugha zao za makabila kama vile kijaluo, kikamba, kikuyu nk. Uwepo wa wasanii mbalimbali kama wale wa kucheza ngoma, kuwepo na waandishi wa habari kwenye sherehe ama mapokezi ya ugeni wa kitaifa au kimataifa ni sehemu ya utamaduni katika jamii fulani. Mapenzi ni hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu au kitu zaidi ya mwingine au kingine. Aidha itikadi ya ubaguzi wa kijinsia imebaishwa katika tasnifu hii. Ubaguzi wa kijinsia ni hali ya kubagua watu kwa misingi ya kijinsia. Jamii nyingi zimekuwa na mtazamo tofauti juu ya watoto wa kiume na kike, wamekuwa wakiwapendelea sana watoto wa kiume na kuwaacha nyuma watoto wa kike. Jamii imekuwa ikikumbatia fikra potofu kwa kuona mtoto wa kiume ndio

mwenye uwezo wa kila kitu na kumdunisha mtoto wa kike kwa kumuona si chochote bali ni chombo cha starehe tu. Ndiege ni mfano mzuri wa wazazi wenye mtazamo kama huu, yeye alimuomba Mungu ampatie mtoto wa kiume ambaye aliamini atakuwa amepata simba atakayekuwa ananguruma tofauti na kupata mtoto wa kike ambaye alimfananisha na ndege tausi ambaye kazi yake ni kupandwa na madume. Mtoto ni mtoto awe wa kiume au kike hivyo wasibaguliwe na wanatakiwa kupata haki zote iwe kutajwa jina. malezi bora na kupatiwa elimu. Musili anamweleza rafiki yake Ndiege, mtoto ni mtoto, awe msichana ama mvulana wote wanastahili kuthaminiwa na kupendwa.

### **5.2.3 Lengo Mahususi la Tatu**

Katika lengo hili kumechambuliwa uhusiano uliopo kati ya siasa na itikadi. Mtafiti ameweza kubaini uhusiano huu kwa kuchambua data zilizojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kama vile masuala ya maendeleo ya kiuchumi, utawala na mfumo wa maisha katika jamii.

Siasa ni njia ya kufanya maamuzi ya jambo lilokusudiwa katika nchi au taifa fulani ambapo itikadi ya chama/nchi itaongoza na kuamua ni aina gani ya uchumi unaofaa kuzalishwa chini ya chama tawala. Kwa mfano, Tom Mboya na Rais Nguruma walikuwa wanaamini itikadi ya kibepari ndio mfumo pekee utakaojenga uchumi wan chi ya Kenya chini ya mshirika wao Marekani (CIA), Mfumo huu ulipingwa na mwanasiasa Mzee Omondi na mwenzake mwanaharakati Abdalla ambapo kiu yao ilikuwa ni kuujenga uchumi wa kijamaa kwa itikadi ya ukoministi waliamini kuwa ni muarubaini wa maendeleo nchini mwao.

Utawala na uongozi bora katika nchi yoyote inategemea siasa na itikadi katika nchi husika kwa maendeleo ya wananchi. Kwa mfano, Abdalla hakuridhika na utawala wa Rais Nguruma kwa kuukumbatia mfumo wa kibepari na siasa za CIA, kitendo hicho kilimfanya kuhama chama na kuhamia chama cha upinzani kwa imani yake chama kimpya kingeleta maendeleo ya haraka katika jamii kuanzia uchumi unaotazamwa kuwa msingi wa mahusiano yote. Lengo kuu ni uzalishaji mali, kuondoa matabaka, katika jamii, kuleta usawa kati ya binadamu na kuwawezesha wanyonge kudai haki zao kwa kuungana.

Siasa na itikadi ndiyo inayoongoza jamii katika kufanikisha mfumo mzima wa maisha katika Nyanja ya uchumi, dini, utamaduni na mwenendo. Kwa mfano, nchini Tanzania chini ya mfumo wa chama kimoja kupitia itikadi ya ujamaa na kujitegemea msingi wake ulikuwa binadamu wote ni sawa na hakuna mtu mwenye haki zaidi ya mtu mwingine. Hivyo mambo haya mawili huongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serikali katika kuongoza na kutawala na kuelekeza namna viongozi wanavyopatikana na viongozi wa namna gani wanahitajika pia kudhibiti masuala yake ya ndani na yale ya nje ili kuleta uwiano sahihi katika jamii husika.

### **5.3 Hitimisho**

Utafiti huu umefanikiwa kukamilisha lengo kuu lililochunguza masuala ya siasa na itikadi yaliyojitokeza katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, lengo kuu liliongozwa na malengo mahususi matatu kupata data sahihi. Lengo mahususi la kwanza lilihusu kubainisha siasa zinazojitokeza katika katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa, tamthiliya *Nyota ya Tom Mboya*

imetawaliwa na masuala ya kisiasa ambayo yalichukua nafasi kubwa katika maisha ya Wakenya na bara zima la Afrika, wanasiasa na wanaharakati wa bara la Afrika walipambana ili kujikwamua kwenye makucha ya ukoloni mamboleo.

Tamthiliya hii inaonyesha siasa zilizojitokeza ni kama vile; siasa na harakati za ujenzi wa jamii mpya, uongozi bora na imani kwa wananchi, ukombozi wan chi za Afrika, elimu na maendeleo, siasa za ukabila, hofu na tama ya madaraka, kujitoa mhanga, nafasi ya mwanamke katika siasa, uhusiano wan chi za Afrika na zile za magharibi na vibaraka wa kisiasa na umwagaji damu. Siasa hizi kwa ujumla wake zilionyesha matukio yaliyokuwa yakifanyika wakati wa ukoloni mamboleo hususani nchini Kenya.

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilihusu kubainisha itikadi alizozitumia mwandishi wa tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*. Utafiti unaonyesha kwamba itikadi mbalimbali zimetumiwa na mwandishi wa tamthiliya hii ili kusawiri maisha halisi katika jamii husika, lengo kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Miongoni mwa itikadi ni kama vile; ushirikina, mapinduzi, ujamaa, ubepari, kikoministi, dini, utamaduni, mapenzi, malezi na uzazi. Matumizi ya itikadi mbalimbali imeweza kutumiwa na mwandishi jinsi viongozi wa bara la Afrika hususani Wakenya wanavyosimamia itikadi zao. Haya yote yamebainishwa vilivyo katika tamthiliya teule.

Lengo mahususi la tatu lilihusu uhusiano uliyopo kati ya siasa na itikadi, kutokana na uchunguzi uliofanywa na mtafiti, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa upo uhusiano

wa karibu kati ya siasa na itikadi kama ifuatavyo; itikadi ni imani au mawazo fulani ambayo ni misingi ya nadharia za mfumo wa kisiasa au kiuchumi wakati siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kundesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii. Ama mbinu ya utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa. Kila chama cha siasa kinaongozwa na itikadi ambayo itakuwa kama dira au mwongozo katika utekelezaji wa malengo yaliyowekwa, aidha utekelezaji huo utazingatia misingi ambayo itajenga uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha katika nchi husika kwa mfano, chama cha kikoministi nchini China inafuata itikadi ya umarx ambayo imekusudia kuleta maendeleo ya haraka katika jamii kama msingi wa mahusiano yote kuanzia uchumi ambapo husisitiza uzalishaji mali, kuondoa matabaka katika jamii, kuleta usawa kati ya binadamu, kuwawezesha wanyonge kudai haki zao kwa kuungana na kuleta mapinduzi dhidi ya wanyonyaji.

#### **5.4 Mapendekezo**

Utafiti ulijikita katika kuchunguza masuala ya siasa na itikadi yaliojitokeza katika tamthiliya ya Mbogo (2016) *Nyota ya Tom Mboya*. Mtafiti amekuwa na mapendekezo yafuatayo;

Kwanza, tafiti zaidi zifanywe katika kuchunguza masuala ya kiuchumi na siasa katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya* kwa kutumia mikabala tofautitofauti ya uhakiki wa kifasihi, hii itatoa mwanga zaidi katika kuelewa masuala ya kiuchumi na kisiasa.

Pili, tafiti zaidi zifanyike katika kuchunguza mbinu mbalimbali za kifasihi na kisanaa zilizotumika katika tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*.

Tatu, kupitia tamthiliya ya *Nyota ya Tom Mboya*, watafiti wengine wachunguze dhamira za kijamii na kisiasa.

### MAREJELEO

- Ambrose, B.M. (2014), *“Kuchunguza Dhamira za Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa Kusadikika na Kufikirika,”* Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Ardono, T. (1950), *The Authoritarian Personality*, New York: Haper.
- Babbie, E., (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Bell, F. (1977), “Marxist Theory, Class Struggle and the Crisis of Capitalism” Jesse Schwartz(ed.), *The Subtle Anatomy of Capitalism*. Sant Monica. Goodyear:
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (2<sup>nd</sup> edition). Oxford: Oxford University Press.
- Chiume, M.W.K.(1980), *Wito wa Kwame Nkrumah: Toleo la Wapigania Uhuru: Panaf Books Limited, London (Toleo la Pili)*
- Chuachua, R.(2011), *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, DaresSalaam: TATAKI.
- Cohen, L. (2000), *Research Methods in Education (5<sup>th</sup> education)*. London.
- Creswell, J. W (2009), *Resarch Design Qualitative and Methods Approches*. Los Angeles: SAGE Publications.
- Engels, F. (1892), *“Introduction” to English edition of Condition of the Working Class in England*. Stanford: Stanford University Press.
- Enon, J. C. (1998), *Education Research, Statistics and Measurement*, Kampala Makerere University.

- Good, G.V. (1966), *Essentials of Educational Research*, New York: Maridith Publications Co.
- Jilala, H (2016), *Misngi ya fasihi linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Daudi Publishing Company. Dar es Salaam.
- Kennedy, E. (1978) *A Philosophe in the Age of Revolution: Destutt de Tracy and the Origins of "Ideology,"* Philadelphia: American Philosophical Society.
- Keys, B. na Wenzake (1989), "*Four face of Full Function Maddle Manger; California Management Review*"; Vol. xxiv. No, 4pp. 59-67
- Kombo, D.K. and Tromp, D.L.A.(2006), *Proposal and Thesis Writing*: Kenya, Panlines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*: New Age International Publishing Ltd.
- Kothari, C.R. (1992:95), *ResearchMethodology: Methods andTechniques (Toleola 2)* NewDelhi: Wiley EasternLtd.
- Loewestein. K. (1953), *The Role of Ideologies in Political Change* "International Social Science Bulletin 5(1): 51-74
- Maina wa Kinyatti (1980), *Thunder from the Mountains: Mau Mau Patriotic Songs*. Zed Press, London.
- Marx, K. (1859) *A Contribution to the Critique of Political Economy*.New York: International Publishers 1970.
- Marx, K. and Engels, F. (1848), "*The Communist Manifesto*" in Marx & Engels Collected Works, Vol. 6, 1845-1848.NewYork: International Publishers
- Mbiti, J. (1956), *The African Philosophy*, London: Oxford University Press.



- Mbogo, E. (2016), *Nyota ya Tom Mboya, Vision Strategic Impact Limited*, Dar es salaam.
- McClosky, H. (1964), Consensus and Ideology in American Politics, *American Political Science Review* 58, 361-82.
- Mlama (Muhando), P. (1991). *Culture and Development: The popular Theatre Approach in Africa*. Nordiska Afrikainstitutet, Uppsala.
- Mlama, P.O (1983), *Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania*, Katika TUKI, *Makala ya Semina III*: 203-222
- Mulokozi, M. and Kahigi, K.K. (1979). *Kungaza Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.
- Mulokozi, M.M (1996), *Fasihi ya Kiswahili: Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: TUKI, Dar es salaam.
- Mutembei, A. K. (2012), *Korasi katika Fasihi*, TATAKI: Dar es Salaam.
- Negri, A. (1982), *Marxbeyond Marx: Notebooks on the Grundrisse*, Forthcoming. New York: I. F. Bergin Press. (Now published by Autonomedia, see: <http://www.autonomedia.org/>).
- Newman, W.L. na Wenzake, (2006). *Social Research*. Sixth Edition, Boston: Pearson.
- Njogu, K. na Chimerah, C. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*: Nairobi Jomo Kenyata Foundation.
- Njogu, K. na Chimerah, C. (2011), *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*: Nairobi Jomo Kenyata Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki Kazi za Fasihi*, Augustana College: Rock Island. IL 61201.
- Nyerere, J. K. (1977a), *Azimio la Arusha Baada ya Miaka Kumi*. Dar es salaam.

- Nyerere, J. K. (1977b), *Azimio la Arusha Baada ya Miaka Kumi*. Dar es salaam.
- Nyerere, J.K (1969), *Ujamaa*, Dar es Salaam. Tanzania.
- Nyerere, J.K (1974), *Binadamu na Maendeleo*: Oxford University Press. Nairobi.
- Nyerere, J.K.,(1968). *Ujamaa: Essays on Socialism*. Nairobi, London and New York: OUP.
- Omari, M. (2011), *Siasa katika Ushairi, Tasnifu ya M.A Kiswahili*, Chuo Kikuu Cha Dar es salaam. Dar es salaam.
- Robson, C., (2007), *How to do a Reserch Project: A Guide for Undergraduate Students*, Carton Victoria: Blackwell Publishing
- Seliger, M. (1976), *Ideology and Politics*, London: George Allen & Unwin. Press
- Semzaba, E (2006), *Tamthiliya ya Kiswahili*, TUKI. Dar es salaam.
- Senkoro, F.E.M.K (1987) *Fasihi na Jamii*. "Uwanja Wa Tahakiki." Dar es Salaam.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982), *Fasihi*, Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.
- Songoyi, E. M (1988). *The Artist and the State in Tanzania, A Study of Two Singers, Kalikali and Mwinamila*, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, (1990), *Elimu ya Siasa*, Dar es salaam.
- TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University: Nairobi
- Wafula, R.M (2003), *Uhakiki wa Tamthiliya; Historia na Maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi. Kenya.
- Wamitila, K. W. (2006), *Uhakiki wa Fasihi, Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide-muwa, Nairobi, Kenya.

WET (1974), *Mtanzania Mpya: Semina ya Uandishi wa vitabu vya Elimu ya Watu*

*Wazima*. Dar es Salaam.

WEU, (1997), *Sera ya Utamaduni*. Dar es Salaam.

Young, P.V. (1984) *Scientific Social Survey and Research*, Englewood Cliffs:

Prentice Hall Inc.